Alhamisi Agosti 24, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581412 www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII




UKURASA 11

tigo pesa SportPesa
MAOKOTO Deilee!
WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



## RIPOTI YA CAG
**Kasoro** tatu kuu zinazodumaza sekta ya elimu zaibuliwa

UKURASA 4

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



Balozi wa Marekani nchini, Michael Battle

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi

# Vyama vya siasa vyatoa msimamo

• **Marekani**, Uswisi: Tunakubaliana na kinachoendelea demokrasia Tanzania... *Uk. 2*

## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

### INDIA YALIPUKA SHANGWE CHOMBO KUTUA MWEZINI

INDIA imelipuka kwa shangwe baada ya chombo chake cha anga za mbali kilichopewa jina la Chandrayaan-3, kutua mwezini huku Waziri Mkuu wake, Narendra Modi, akisema...

## Mashahidi wawili wakwamisha kesi mauaji ya dada wa Bilionea Msuya

UKURASA 5




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, akionyesha kwa waandishi wa habari (hawapo pichani) ndoo iliyo na mawe ya madini ya dhahabu yenye uzito wa gramu 6,753.4, thamani yake Sh. bilioni 9.2, yaliyokamatwa yakitoroshwa baada ya kuibwa katika Mgodi wa Dhahabu Bulyanhulu, mkoani humo jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Madini ya bil. 9.2/- yaliyoibwa yanaswa

UK.7

**MICHEZO** YANGA YAKAMILISHA MAWINDO YA ASAS UK.24 **KATUNI** UK.6



Rundo la taka likiwa katika eneo la Vingunguti jijini Dar es Salaam jana ambazo zimetelekezwa kwa muda mrefu bila kuzolewa na mamlaka, zinasababisha usumbufu kwa wakazi wa eneo hilo na watumiaji wa barabara. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## ...Marekani, Uswisi wasema wanakubaliana demokrasia

**Na Halfani Chusi**

MABALOZI wa Marekani na Uswisi nchini, wamesema demokrasia inapaswa kuangalia mazingira ya nchi, huku wakipongeza kukua kwa demokrasia Tanzania. Kumeiweka nchi katika nafasi nzuri duniani.

Mabalozi hao waliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa kitaifa wa wadau kujadili hali ya demokrasia nchini kuelekea uchaguzi wa 2024 na 2025.

Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassot, alisema safari ya miaka 30 ya demokrasia ya vyama vingi hadi sasa haionekani kuwa rahisi wala kunyooka, lakini kwa Tanzania inaonyesha mabadiliko makubwa kwa sasa.

Alisema kuna kipindi demokrasia ilishuka kidogo, lakini kwa sasa hali imeanza kuwa shwari kutokana na juhudi zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Uswisi inaipongeza serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhimiza kikamilifu demokrasia kwa kuhudhuria mikutano mingine ya vyama vya siasa na vile vya upinzani.

"Tunajivunia sana na kushangilia kwamba Rais Samia alihudhuria mkutano uliopita wa demokrasia, kitendo hicho kiliweka mwelekeo wa mustakabali wa demokrasia ya Tanzania.

"Ni muhimu kutambua kwamba kila demokrasia haifanani, haipaswi kufanana. Lazima iwe na mazingira yake. Demokrasia ya Tanzania inaweza isiwe na matawi huru, lazima iakisi nchi yake, iwe ya kipekee, iwe na ukungu iliyojitengenezea. Hakuna taifa katika sayari ya dunia lenye haki ya kuitamkia Tanzania demokrasia yake iweje," alisema.

Balozi wa Marekani nchini, Michael Battle alisema ni muhimu demokrasia iangalie mazingira ya Tanzania na ifanane na Tanzania huku akipongeza serikali kwa kuweka jitihada pamoja kwa kushirikisha wadau kukuza demokrasia.

Alisema Tanzania imekuwa ikipiga hatua vizuri na wao (Marekani) wataendelea kuwa washirika wa Tanzania ili kusaidia kukuza demokrasia kutokana na matokeo mazuri yanayoonekana.

Marekani na Uswisi ni miongoni mwa wadau waliofadhili mkutano huo ambao kwa mwaka huu mgeni rasmi alikuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

# Vyama vya siasa vyatoa msimamo

**Na Halfani Chusi**

VYAMA vya siasa vimetoa msimamo kwamba ni muhimu uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na uchaguzi mkuu wa 2025 ukafanyika kukiwa na mabadiliko ya sheria na kuruhusu matokeo ya urais kuhojiwa mahakamani.

Aidha, vyama hivyo kupitia Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) vimetaka kuwapo Tume Huru ya Uchaguzi, mgombea binafsi na wasimamizi ambao hawatoki Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na haki. Pia vimependekeza uchaguzi wa serikali za mitaa kusimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi badala ya TAMISEMI.

Akisoma maazimio mbele ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, katika mkutano wa kitaifa wa kujadili hali ya demokrasia nchini kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu, Mwenyekiti wa TDC, Prof. Ibrahimu Lipumba, alisema lengo ni kuwa na uchaguzi wenye tija.

Lipumba alisema vyama vya siasa na wadau wanaona ni muhimu kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi, mgombe binafsi na kuruhusu matokeo ya urais kuhojiwa mahakamani, ikiwa ushindi wake utatiliwa shaka.

Pendekezo lingine ni wadau wa maendeleo na serikali kuendelea kutoa elimu ya demokrasia kwa umma kuhusu umuhimu wa kupiga kura hasa katika wakati ambao idadi ya wapigakura inapungua.

Aidha, wametaka marekebisho ya sheria kuruhusu wanaotoka kwenye utumishi wa umma kwenda kugombea wanaposhindwa warudi kazini katika nafasi zao za awali. Lengo ni kuwapatia nafasi wananchi hasa wanawake kuchangamkia nafasi za siasa bila kuhofia kupoteza kazi.

"Wanawake washirikishwe kwenye vyombo vya uamuzi kwenye ngazi za juu za kisiasa. Kuondoa kigezo cha kulipia fomu ya urais Sh. milioni moja kwa kuwa kuna wanaokosa fedha hizo lakini wana sifa," alisema.

Lipumba alisema ni muhimu viongozi wa vyama vya siasa kuepuka lugha zisizo za staha bali wajenge hoja zitakazoisaidia serikali na kuiletea nchi mabadiliko. Pia alitaka kuweka mazingira mazuri ya kuwa na uchaguzi huru na haki na utakaofanyika kwa amani bila kuingiliwa na vyombo va dola.

### KUBORESHA UCHAGUZI

Vyama vya upinzani, vilitoa mapendekezo ya kuboresha uchaguzi ujao wa serikali za mitaa 2024 na uchaguzi mkuu 2025.

Akifungua pazia la hoja, Kiongozi wa ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema ili kuboresha uchaguzi ujao, serikali inapaswa kuhusishwa na namna uchaguzi unavyofanyika na kupatikana kwa katiba mpya.

Alishauri Sheria ya Tume ya Uchaguzi ihusishe uchaguzi wote huku akiisihi serikali kukaa na wadau na kukubaliana ipelekwe bungeni ijadiliwe ili sheria itumike.

"Tukiendelea na mijadala kianze hiki mara kile, haya mambo yana mlolongo mrefu hatutamaliza leo na uchaguzi umekaribia. Pamoja na kwamba tunahitaji Katiba Mpya, tume huru ya uchaguzi ni muhimu ipatikane mapema ili itumike," alisema.

Pia alishauri Zanzibar iachane na utamaduni wa kupiga kura kwa siku mbili kwa kile alichosema ni chanzo cha machafuko na mauaji yanayotokea kipindi cha uchaguzi.

"Iletwe miswaada yote miwili kwenye mkutano mmoja wa bunge tukiruhusu mmoja uje halafu mwingine tuujadili baadaye tutatumia muda mwingi na mwisho wa siku tutachelewa kupata suluhu," alishauri.

Mwakilishi kutoka NCCR Mageuzi, Faustine Sungura, alikumbushia kauli ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, iliyosema "hatuwezi kufikiria mambo mema mapya kama tunaendelea kufikiria mabaya ya zamani."

Mkurugenzi wa Mikakati wa CHADEMA, Reginald Munisi, alisema ni wakati mwafaka kuanza na mabadiliko ya sheria na Tume Huru ya Uchaguzi kwa kuwa wananchi hawana imani na uchaguzi.

"Elimu itolewe kwa ukubwa. Watu wajue umuhimu wa kupiga kura na wawe na imani na uendeshaji wake. Mashirika yasiyo ya kiserikali, vyama vya siasa, mashirika ya dini na wadau mbalimbali washiriki kutoa elimu ili kuwaongezea uelewa," alisema.

Kamishna wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Hamisi Isa Hamisi, alisema ili kupata uchaguzi bora lazima serikali iwekeze zaidi kwenye elimu kwa wapigakura na kuandaa mpango kazi na fedha.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Anamringi Macha, alisema mchakato wa Katiba Mpya iliyopendekezwa ulikwama kwa sababu vyama vingi vya siasa havikufikia maridhiano.

Kuhusu Katiba mpya alisema haiandikwi kama kitabu cha hadithi bali ni jambo linalowahusu wananchi na ni mchakato mrefu unaohitaji kukidhi mahitaji yao.

"Kwa sasa tungehangaika kurekebisha baadhi ya vipengele vilivyomo kwenye katiba kuhusu uchaguzi kwa sababu ndilo jambo ambalo liko jirani. Hatuwezi kushughulikia katiba wakati tuna mambo mengi ya uchaguzi.

"Watanzania wanapaswa kufahamu tunaye kiongozi mwenye dhamira thabiti ambaye ni Rais Samia Suluhu Hassan ndiyo maana unaona kwa sasa kuna demokrasia. Utashi wetu uwe kwa kila chama ikiwamo kutoa elimu na kuyamulika maeneo mengine ili kuboresha uchaguzi," alishauri.

### MSAJILI, MWINYI WANENA

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, alisema sheria za uchaguzi zilizopo kuna wakati zinakuwa na upungufu. Alisema ili kuwa na uchaguzi bora, inapaswa kusimamiwa na viongozi wenye maadili akitolea mfano kwamba baadhi yao hujihusisha na vitendo vya rushwa.

Alisema wakiwa walezi wa vyama hivyo wataendelea kuvifanya kuwa taasisi imara na kuenzi demokrasia kwa kuvisaidia kutii sheria na utaratibu uliowekwa ili kuendelea kulinda amani na umoja wetu.

Akizungumza kwa niaba ya Rais Samia, Dk. Mwinyi alisema serikali imeyabeba na itayafanyia kazi mapendekezo yote yaliyotolewa.

Pia alisema serikali itaendelea kudumisha demokrasia akitolea mfano hata kufanyika kwa mkutano huo ni ishara ya kuwapo kwa demokrasia, umoja na mshikamano.

HABARI KITAIFA

## India yalipuka shangwe chombo kutua mwezini

**Na Restituta James**

INDIA imelipuka kwa shangwe baada ya chombo chake cha anga za mbali kilichopewa jina la Chandrayaan-3, kutua mwezini huku Waziri Mkuu wake, Narendra Modi, akisema: "India iko mwezini."

Jana nchi hiyo iliweka rekodi ya kupeleka chombo hicho mwezini ambacho kiligusa ncha ya kusini ya mwezi majira ya saa 9:00 alasiri kwa saa za Afrika Mashariki.

Shangwe za raia wa India ambao walishuhudia jaribio hilo moja kwa moja kupitia mitandao ya kijamii, limetokana na kushindwa kwa Chandrayaan-2, iliyoanguka mwaka 2019. Vyombo vya habari vya kimataifa viliripoti jana kwamba maofisa katika makao makuu ya Shirika la Anga za Juu la India (ISRO) lenye makao yake Bengaluru, walishangilia baada ya chombo hicho kuanza kuteremka wima kwa nguvu kwenda mahali kilipotua.

Mafanikio ya ISRO yanaiweka India kwenye nafasi ya nne ya nchi zilizofanikiwa kupeleka chombo mwezini baada ya Marekani, China na Russia.

Hata hivyo, India imepata sifa ya pekee kwenye kumbukumbu ya kwenda mwezini baada ya kuwa ya kwanza kugusa upande wa kusini wa mwezi.

Mamilioni ya watu kote India na duniani, walifuatilia kwa karibu tukio hilo lililokuwa likisubiriwa kwa hamu, Shirika la Habari la India (ANI) liliripoti.

ISRO ilirusha tukio hilo moja kwa moja kwenye tovuti yake na mitandao yake ya kijamii pamoja na televisheni ya taifa nchini humo. Chombo hicho kilianza safari yake Agosti 5, mwaka huu, baada ya kuingizwa kwa mafanikio kwenye mzunguko wa mwezi.

Mwanzilishi wa mpango wa Chandrayaan-3 amepewa jina la Vikram Sarabhai (1919–1971), ambaye anatajwa kama baba wa mpango wa anga za juu wa India.

# Mwili wa mwalimu aliyepotea wakutwa mashamba ya miwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MWALIMU wa Shule ya Awali Kill Hope, Lightness Elia (20), ambaye alipotea Julai 20, mwaka huu, katika mazingira ya kutatanisha, mwili wake umekutwa ukifukuliwa na mbwa katika eneo la mashamba ya TPC.

Elia alikuwa akiishi nyumbani kwa mjomba wake, Justine Urio, eneo la Matindigani kunakotazamana na shamba la miwa la TPC.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Shaaban Hamza, alisema baada ya kusikia mbwa wanabweka kwa muda mrefu, walisogelea eneo hilo na kukuta kiwiliwili cha binadamu kisha wakatoa taarifa kwa viongozi wa mtaa ambao waliwajulisha polisi na baadaye ndugu waliutambua mwili huo.

"Polisi waliwasiliana na ndugu waliobaini uwezekano ni mwalimu huyo kutokana na nguo, viatu, pochi na kibegi ambavyo walivitambua," alisema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Relini, Elizabeth Mputa, alisema alifika eneo la tukio na ndugu wa marehemu walimtambua ndugu yao.

Akizungumzia kupotea kwa mwalimu huyo, mmliki wa Shule ya Kill Hope, Sadiki Stephan, aliliambia Nipashe kuwa Julai 20, majira ya saa 2:00 usiku alipata simu kutoka kwa rafiki wa marehemu (aliyemuunganisha kwake kupata kazi) akimpatia taarifa kuwa bado mwalimu huyo hajafika nyumbani kinyume cha ilivyozoeleka.

"Nilishangaa na kwa kuwa nina ofisi mbili nililazimika kumpigia mke wangu ili kujua kama mwalimu huyo alionekana shuleni kwa siku hiyo. Walinijulisha kuwa hakufika shuleni kwa siku hiyo na watoto walifika shuleni na hadi muda wa kutoka mwalimu wao hakuonekana na wala simu zake zilikuwa hazipatikani. Nilimrudia rafiki yake na kumjuza taarifa hizo na kuendelea kumtafuta kwa kushirikiana na familia," alisema.

Baba mzazi wa binti huyo, Elia Makyao, alisema mwanawe alitoweka nyumbani kwa mjomba wake alipokuwa anaishi na ilidaiwa alitoka na kwenda shuleni huku mwajiri wake akidai kuwa hajafika.

"Nilipewa taarifa siku hiyo jioni na kesho yake asubuhi, nilifika nyumbani hapo na kukuta mjomba wake ametoka. Nilifanya mazungumzo na vijana wa bodaboda, ambao wako jirani na eneo la nyumba hiyo wakanieleza kuwa Julai 20 hawakumwona akienda shuleni ingawa nyumbani alipokuwa akiishi alifahamishwa kuwa alitoka na kwenda shuleni kama kawaida ingawa hakurudi.

"Tulipofika chumbani kwake, tulikuta chumba kimevurugwa hakijafanywa usafi, wala kutandikwa ila mjomba wake aliniambia kwa njia ya simu binti huyo aliamka siku hiyo na kufanya usafi kisha kuondoka kwenda shuleni. Mimi sijui ukweli ni upi ila nimemtafuta binti yangu kwa nguvu zangu zote bila mafanikio. Nilipewa RB namba MOS/RB/608/2023,"alisema.

"Nilianza kumsaka ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwa viongozi wa mtaa pamoja na jeshi la polisi ingawa sikupata ushirikiano kutoka kwa mmoja wake hata kuulizwa umefikia wapi au nini kifanyike na badala yake mtoto wa mjomba huyo," aliongeza.

Mjomba wa marehemu, Urio alisema anachojua ni kwamba mtoto huyo alitoka asubuhi kwenda shuleni anakofanya kazi na hajui chochote.

"Ni kweli nakaa naye nyumbani kwangu ila ana chumba chake. Aliamka akafanya usafi kama kawaida yake na kisha kwenda kibaruani. Jioni ilipofika tulimtafuta bila mafanikio na tukamjuza baba yake, hivyo tulijua ipo siku atarudi maana hakubeba chochote. Alikuwa binti mtulivu, hana mambo ya wanaume wala tabia mbaya. Hatujui ni nini kimetokea labda kama ni visasi vya familia yao mimi siwezi kujua,"alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP) Simon Maigwa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema uchunguzi wa kina unafanyika kubaini ukweli wa jambo hilo.




Madereva wa bodaboda wakiwa wamezuia daladala isipite wakimtuhumu dereva wake kusababisha ajali kwa kumgonga mwenzao, eneo la Keko Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TANESCO yasema tatizo la umeme limekwisha

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limesema hitilafu ya mfumo katika kituo cha uzalishaji umeme kwa njia ya gesi cha Ubungo II iliyotokea juzi imetatuliwa.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi wa Huduma kwa wateja wa shirika hilo, Martin Mwambene, tayari huduma ya umeme imerejea kama kawaida nchi nzima.

Juzi shirika hilo lilitoa taarifa ya hitilafu hiyo iliyosababisha upungufu wa uzalishaji umeme kwa jumla ya megawati 268 kutokuwa kwenye mfumo wake wa usafirishaji na baadhi ya maeneo kwenye mikoa kukosa huduma hiyo kwa nyakati tofauti.

Aidha, jana Ofisi ya Uhusiano na Huduma kwa wateja TANESCO Kinondoni Kaskazini, ilitoa taarifa iliyoeleza kwamba kutokana na hitilafu na matengenezo yaliyoendelea katika kituo cha uzalishaji umeme kwa njia ya gesi cha Ubungo II, ilisababisha kuwapo na upungufu wa umeme kwa baadhi ya maeneo kwa mkoa huo.

Baadhi ya maeneo yaliyotajwa kukosa umeme kwa jana ni Zena Kawawa, Shoppers Plaza, Maguruwe, Kwa Apson, Rungwe Street, Rainbow, Top Garage, JK Nyerere, Ruvent Street, Ambrosia, Kwa Mboma, BoT quarters, Bahari Beach, Ras kilomon, Unio na Kondo,

Mengine ni baadhi ya maeneo ya Boko, Boko Magengeni, Boko NHC, Burumawe, Boko kwa Wagogo, Dogodogo Center, Boko Maliasili, Boko Dovya, Boko Magereza, Boko Machimbo na Boko Mwangalani.

Pia, Mbweni NHC, Mbweni JKT, Mbweni Kijijini, Mbweni Malindi, Mbweni Ubungo na baadhi ya maeneo ya Mbweni Teta, Kinondoni yote, Ananasifu, Mkwajuni, Biafra, Makaburini, Kawe, Moyo Health Clinic, Moscow, Kwa Pinda, Open University, Chama cha Walimu, Tibaijuka Street, Morocco na maeneo ya jirani.

"Mara matengenezo yatakapokamilika huduma ya umeme itarejea katika hali ya kawaida kwa maeneo yote. Shirika linawashukuru wateja wake kwa uvumilivu katika kipindi chote ambacho huduma ya umeme ilikosekana," ilieleza taarifa hiyo.


UCHAMBUZI RIPOTI YA CAG

# Taasisi yaibua kasoro tatu kuu sekta ya elimu

• Viwango duni walimu kusimamia miradi ya ujenzi



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ludovick Utouh.

**Na Mwanahamisi Mussa,** TUDARCo

TAASISI ya WAJIBU imechambua ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2021/22, ikibaini kasoro kubwa tatu katika Sekta ya Elimu, ikiwamo ufaulu usioridhisha katika baadhi ya shule za serikali, huku walimu wakipewa jukumu la kusimamia miradi ya ujenzi ilhali hawana utaalamu huo.

Katika ripoti yake ya uchambuzi aliyoipa jina la 'Ripoti ya Uwajibikaji - Utoaji wa Huduma kwa Jamii', taasisi hiyo inabainisha kuwa kwa mwaka huo wa ukaguzi, katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (halmashauri) 96, wanafunzi 158,185 sawa na asilimia 66 ya waliofanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne mwaka wa masomo 2021/22, walipata daraja la nne na sifuri.

Taasisi hiyo inayoongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Ludovick Utouh - CAG mstaafu, inafafanua katika ripoti yake ya uchambuzi kwamba, ili kuonesha hali ya utoaji wa huduma kwa jamii kwa mwaka 2021/22, imefanya uchambuzi wa hoja mbalimbali za CAG ambazo zimeonesha hali halisi ya utoaji wa huduma za kijamii, ikishauri namna ya kuboresha mazingira ya utoaji wa huduma hizo nchini.

WAJIBU inabainisha kuwa uchambuzi wake huo umezingatia mikoa 19 ambayo iko katika mpango kazi wa utekelezaji wa shughuli zake. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Njombe, Iringa, Ruvuma, Mtwara, Dodoma, Tanga, Mbeya, Kilimanjaro, Arusha, Pwani, Tabora, Rukwa, Singida, Katavi, Morogoro, Mwanza, Manyara na Kigoma.

> **Lengo hili ni sawa na Azimio la Incheon la mwaka 2015 linazozitaka nchi zilizo ukanda wa kusini mwa Jangwa la Sahara kutenga angalau asilimia 20 ya bajeti ya taifa kwa ajili ya Sekta ya Elimu.**

Uchambuzi wa taasisi hiyo pia umehusisha miradi ya sekta za elimu, maji, afya na kilimo. Katika Sekta ya Elimu, taasisi hiyo inaeleza kuwa kupitia

Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano (2020/21-2025/26), serikali imepanga kuongeza bajeti ya sekta ya elimu kutoka asilimia 18.7 ya bajeti ya taifa ya mwaka 2021/22 hadi kufikia asilimia 20 ifikapo mwaka 2025/26.

"Lengo hili ni sawa na Azimio la Incheon la mwaka 2015 linazozitaka nchi zilizo ukanda wa kusini mwa Jangwa la Sahara kutenga angalau asilimia 20 ya bajeti ya taifa kwa ajili ya Sekta ya Elimu.

"Kwa mwaka 2021/22, Bunge liliidhinisha bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya kiasi cha Sh. trilioni 5.26, ambayo ilikuwa asilimia 14.3 ya bajeti ya taifa kwa mwaka husika. Hiki ni kiwango kidogo kulinganisha na asilimia 20 iliyokubaliwa kimataifa.

"Hata hivyo, Wizara ya Elimu ilipokea jumla ya Sh. bilioni 994.71 sawa na asilimia 96 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta ya elimu kwa mwaka 2021/22," WAJIBU inabainisha katika ripoti yake hiyo.

Hata hivyo, taasisi inasema inatambua serikali kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia (WB), inatekeleza programu ya kuboresha elimu ya sekondari (SEQUIP) katika halmashauri zote 184 yenye thamani ya Sh. trilioni 1.15, ili kusaidia kutatua changamoto ya uhaba wa majengo katika shule za sekondari nchini.

### DOSARI ZILIZOPO

Pamoja na uwekezaji ambao serikali imefanya katika kuhakikisha wanafunzi wanapata mazingira mazuri ya kusomea, WAJIBU inafafanua kuwa CAG amebaini changamoto zinazoathiri ubora wa miradi ya elimu nchini, ikiwa ni pamoja na ukaguzi na usimamizi usioridhisha wa miradi ya ujenzi.

Dosari nyingine ni utaratibu wa kutumia walimu kusimamia na kukagua miradi ya ujenzi inayotekelezwa katika sekta ya elimu ambao ni kinyume cha Mwongozo wa Kutekeleza Kazi za Ujenzi kwa Njia ya Kutumia Uwezo wa Ndani Katika Utekelezaji wa Miradi (Force Account) wa Mei 2020.

Mwongozo unamtaka Mkurugenzi wa Halmashauri kwa kutumia wataalamu wa halmashauri, kusimamia utekelezaji wa mradi hiyo. Mwongozo huo pia unaelekeza Mhandisi wa Halmashauri kuwa na jukumu la kusimamia shughuli za ujenzi za kila siku.

"Kushindwa kutekeleza mwongozo huu kwa baadhi ya halmashauri, kumesababisha miradi kusimamiwa na walimu na wanajamii wasio na utaalamu wa masuala ya ujenzi, hivyo kuathiri ufanisi na ubora wa majengo hayo," inasema taasisi hiyo katika ripoti yake ya uchambuzi.

Taasisi ya WAJIBU pia inaimulika dosari ya ukosefu wa uhalisia wa bajeti ya ujenzi wa shule za sekondari, ikibainisha kuwa ujenzi wa shule mpya za sekondari 59 sawa na asilimia 50 ya shule zilizotengewa fedha za UVIKO 19, haukuwa umekamilika na fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo, zote zilikuwa zimetumika.

### MADHARA

Taasisi hiyo inabainisha kuwa dosari hizo zinasababisha mazingira duni ya kufundishia na kujifunza, hivyo kuwa na ufaulu usioridhisha katika baadhi ya shule za serikali.

"Kwa mwaka 2021/22, katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 96, wanafunzi 158,185 sawa na asilimia 66 ya waliofanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne mwaka wa masomo 2021/22, walipata daraja la nne au sifuri," inabainisha taasisi hiyo.

WAJIBU pia inaangazia madhara mengine yanayojumuisha kukatisha masomo kwa baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, ikibainisha kuwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 11, wanafunzi 19,945 sawa na asilimia 25 ya wanafunzi waliosajiliwa mwaka 2015, hawakumaliza darasa la saba mwaka 2021/22.

Vilevile, katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 19, wanafunzi 22,039 sawa na asilimia 28, waliojiunga na kidato cha kwanza mwaka 2018/19, hawakufanikiwa kukamilisha elimu ya kidato cha nne.

"Pia kuna dosari ya miundombinu isiyojitosheleza kwa shule za msingi na sekondari. Kwa mwaka 2021/22, Mamlaka za Serikali za Mitaa 45 zilikuwa na upungufu wa miundombinu kama vyoo vya wanafunzi, nyumba za waalimu, mabweni, maktaba, vyumba vya kompyuta, majengo ya utawala na maabara.

"Upungufu mkubwa wa miundombinu kwenye shule za msingi umeonekana zaidi katika nyumba za walimu (asilimia 78) na vyoo vya wanafunzi (asilimia 56), Kwa sekondari umeonekana zaidi katika nyumba za walimu (asilimia 81), maktaba (asilimia 84), vyumba vya chakula (asilimia 84) na vyumba vya kompyuta (asilimia 80)," inafafanua taasisi hiyo.

### NINI KIFANYIKE?

WAJIBU inapendekeza katika ripoti yake hiyo kuwa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Bunge na Serikali Kuu kuacha kutumia walimu kusimamia ujenzi wa miundombinu shuleni kwa kuwa hawana utaalamu na ujuzi wa shughuli hizo ambazo ni za kitaalamu.

Taasisi hizo pia ziinapendekeza kamati za shule na Bodi za Usimamizi wa Shule ziendelee kupewa mafunzo kuhusu majukumu yao, pia zishirikiane na uongozi wa serikali ya kijiji katika kusimamia na uangalizi wa ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari.

"Tunapendekeza kuhuisha makadirio ya gharama za ujenzi ili kuzingatia uhalisia wa maeneo husika na muda wa ujenzi. Kumekuwapo utoaji fedha za ujenzi wa shule/madarasa/maabara kwa kiwango kinacholingana kwa shule zote nchini.

"Bunge, katika kuhimiza utekelezaji wa mapendekezo ya CAG, liitake serikali kusimamia ipasavyo utekelezaji wa miongozo na matakwa ya kimataifa kuhusu ugharamiaji wa elimu kwa kutenga asilimia 20 ya bajeti ya nchi au asilimia sita ya Pato Ghafi la Taifa (GDP) kwenda katika Sekta ya Elimu.

"Serikali iongeze ufanisi na tija katika kusimamia mapato na matumizi yake kwa kupunguza upotevu wa mapato na matumizi yasiyo na tija. Kwa kufanya hivyo, serikali itaongeza uwezo wake wa kutoa fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa katika sekta ya elimu," Taasisi ya WAJIBU inashauri katika ripoti yake hiyo.

Ripoti ya CAG kwa mwaka 2021/22 iliwasilishwa bungeni Aprili 6 mwaka huu baada ya CAG Charles Kichere kuikabidhi kwa Rais Samia Suluhu Hassan mwishoni mwa mwezi Machi mwaka huu.

## Wahukumiwa kisa kwenda 'Sauzi'

**Na Neema Msalaba,** TUDARCo

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imewahukumu Watanzania 28 kulipa faini ya Sh. 70,000 kila mmoja au kwenda jela miaka miwili baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kutoka nchini na kwenda kuishi Afrika Kusini bila kufuata utaratibu.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, baada ya washtakiwa kukiri makosa yao.

"Kwa kuwa mmekiri makosa yenu, mahakama inawahukumu kulipa faini ya Sh. 70,000 kila mmoja au kwenda jela miaka miwili ili mkafundishwe namna sahihi ya utafutaji kwa kuwa hata nchini kuna hali nzuri ya mtu kujitafutia kipato. Wengine ndugu zenu walijua mmeshafariki dunia na kitendo hicho mlichofanya si cha busara," alisema.

Wakili wa Serikali Mwandamizi Shija Sita, alidai raia hao wa Tanzania walikamatwa Agosti 20 mwaka huu Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), jijini Dar es Salaam, kwa kosa la kutoka nchini na kwenda Afrika Kusini kinyume cha sheria.

Vilevile, ilidaiwa mahakamani huko kuwa tarehe hiyohiyo, washtakiwa walifikishwa ofisi za Jeshi la Uhamiaji na kuchukuliwa maelezo na wote walikiri kutenda kosa hilo na Agosti 22 mwaka huu, walifikishwa mbele ya mahakama hiyo ili kujibu mashtaka dhidi yao.

"Ninaomba mahakama itoe adhabu kali kwa sababu serikali imetumia gharama kubwa za kuwasafirisha na chakula kutoka huko mpaka kuwafikisha hapa mahakamani," alidai Shija.

Washtakiwa hao baadhi yao waliomba mahakama iwaonee huruma na kuwasamehe. Wengine waliomba wapunguziwe faini kutokana na familia zao kuwa na uwezo mdogo na wengine kwa Dar es Salaam hawana ndugu na hawajui eneo walikokuwa.

# Mashahidi wakwamisha kesi ya dada wa Bilionea Msuya

**Na Grace Gurisha**

KESI ya mauaji ya mdogo wa marehemu, Erasto Msuya 'Bilionea Msuya', Aneth Msuya, imeahirishwa kusikilizwa kutokana na mashahidi wawili wa upande wa mashtaka kushindwa kufika mahakamani.

Washtakiwa katika kesi hiyo namba 103 ya mwaka 2018, ni mke wa aliyekuwa mfanyabiashara huyo maarufu wa madini mkoani Arusha - Bilionea Msuya, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela, wote wakazi wa mkoani Arusha.

Jana, shahidi wa 21 wa upande wa mashtaka alitakiwa kutoa ushahidi wake mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, lakini ilishindikana kutokana na mashahidi waliokuwa wanategemewa kwa wiki hii, kupata changamoto.

Wakili wa Serikali Paul Kimweri alidai mashahidi waliopangwa kwa wiki hii ni wawili; shahidi wa kwanza ni WP 5412 Sajenti Mwaka na ASP Jumanne Marangae ambao hao ndiyo walikuwa wanafunga kwa wiki hii.

"Kwa bahati mbaya, upatikanaji wa hawa mashahidi wote wawili umekuwa mgumu. Huyu Mwaka, barua ya wito wake imeandikwa na Askari Seba kwa kuambatanishwa na nyaraka ambazo zinaelezea kutokuwapo kwake.

"Bado yupo likizo ya uzazi ambayo inaisha Septemba Mosi mwaka huu. Aliitwa wiki hii kwa sababu likizo yake ilikuwa inakaribia kuisha, lakini alisema angeweza kuja hata kabla ya tarehe hiyo, lakini amepata changamoto ya uti wa mgongo. Kwahiyo, hali yake ya kiafya ameshindwa kuhudhuria," alidai.

Wakili Kimweri alidai shahidi mwingine ASP Marangae ni mpelelezi wa kesi hiyo, lakini kwa sasa ana majukumu mengine. Ni Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kagera.

"Kutokana na nafasi hiyo tumekutana na changamoto ya upatikanaji wake. Changamoto tuliyokutana nayo ni yeye kuwapo kwenye kikosi kazi na yeye kama Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa alipaswa kuwapo, ikatokea shahidi huyu kushindwa kufika kwa wakati.

"Tumeshindwa kuwapata, lakini wametuahidi kwamba watakuwapo wiki ijayo. Hatuwezi kuwapata mashahidi wengine kwa sababu tumewaita kwa 'samasi' za wiki ijayo na wanatoka mbali. Kama wangekuwa ni wa Dar es Salaam, tungewaandikia barua waje," alidai.

Kimweri aliomba mahakama iridhie kuwapa ahirisho hadi wiki ijayo Jumatatu ili kuendelea kutoa ushahidi kwa mashahidi wao alioahidi watakuwepo mahakamani.

Baada ya Kimweri kudai hayo, Wakili wa Utetezi Peter Kibatala alidai hawana pingamizi, lakini anaamini kwamba kwa wiki ijayo watafidia hizo siku tatu zilizopita pasi na kuendelea kusikilizwa kesi hiyo.

"Kutokana na sababu zilizotolewa, mahakama haina mbadala mwingine ni kuahirisha tu hadi Agosti 28 mwaka huu, ambapo upande wa mashtaka unaelekezwa kuhakikisha wiki ijayo wanaendelea na shauri hili, kwa kipindi hicho washtakiwa wataendelea kukaa ndani," Jaji Kakolaki alisema.

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji ya wifi yake ya Mei 25, 2016, akiripotiwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake, Kibada, wilayani Kigamboni, mkoani Dar es Salaam, amekiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo.




Mkurugenzi Mtendaji wa NIC Insurance, Dk. Elirehema Doriye (katikati), akiwa na Mkurugenzi wa Masoko na Mawasiliano, Karim Meshack (kushoto) na Mkurugenzi wa Fedha na Uwekezaji, Lihami Masoli, wakisherehekea kampuni hiyo ya serikali kupatiwa cheti cha Usimamizi wa Ubora wa Kimataifa (ISO), jijini Dar es Salaam jana. NIC imeshashinda takribani tuzo 7 kwa mwaka huu pekee na hivi karibuni ilipokea tuzo ya utendaji bora katika sekta za fedha na ya ubora wa huduma za bima ya Superbrands kwa Ukanda wa Afrika ya Mashariki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ujenzi kampasi Chuo Kikuu Dar es Salaam waiva

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imetangaza kuwa Desemba mwaka huu, ujenzi wa kampasi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) utaanza rasmi huko Gongo, Kata ya Jamhuri, mkoani Lindi.

Imesema hatua hiyo itawawezesha kupanua wigo wa upatikanaji wa elimu ya juu nchini, uamuzi huo ukitangazwa jana na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alipokagua eneo la ujenzi wa kampasi hiyo unaotekelezwa kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).

Waziri Mkenda alisema kujengwa kampasi hiyo ni maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha mikoa yote ambayo haina vyuo vikuu inajengewa kampasi za vyuo vikuu kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa elimu kwa urahisi zaidi.

"Leo (jana) nimekuja kutangaza rasmi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimekamilisha taratibu za kikanuni na kisheria za kuanzisha kampasi. Kutakuwa na kampasi ya chuo hicho hapa Lindi na kitaanza na wanafunzi 360," alisema Prof. Mkenda.

Aliitaja mikoa mingine itakayojengewa kampasi za vyuo vikuu chini ya mradi huo kuwa ni Kagera, Mwanza, Shinyanga, Singida, Manyara, Tanga, Simiyu, Kigoma, Ruvuma, Rukwa, Katavi na Zanzibar (Institute of Marine Scince).

Waziri Mkenda alivitaka vyuo vikuu vyote vitakavyojenga kampasi hizo, kuzielekeza katika kutoa mafunzo ya amali na kufanya utafiti huku akiahidi kutoa ushirikiano mkubwa.

Wananchi wameipongeza serikali kwa uamuzi huo na kuwashirikisha katika hatua zote. Wanaamini utaleta mabadiliko makubwa ikiwamo kuchochea maendeleo.

Waliiomba serikali kuhakikisha mkandarasi atakaopewa kazi ya ujenzi huo anaifanya kwa weledi na kwa wakati.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack, Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, aliishukuru serikali kwa uamuzi huo ambao ulisubiriwa kwa hamu na wananchi wa Lindi na mikoa jirani.

Alisema mkoa umewezesha upatikanaji eneo la zaidi ya ekari 492 na wataendelea kutoa ushirikiano ili ujenzi utakapoanza, ukamilike kwa wakati.

Naibu Makamu Mkuu wa UDSM (Mipango, Fedha na Utawala), Prof. Bernadetha Killian, alisema kupitia mradi wa HEET, chuo kimepata Dola za Marekani milioni 47.5 kwa ajili ya kutekeleza mradi kupitia shughuli mbalimbali na kitajikita zaidi katika masuala ya kilimo na ufugaji nyuki. Pia kitakuwa na kituo wilayani Ruangwa, mkoani Lindi kwa ajili ya mafunzo ya vitendo na utafiti.

***Imeandaliwa na Salma Chindole (SAUT) na Julieth Ng'oma (TUDARCo)***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mkataba wa ushirikiano Tanzania, Indonesia ulete matokeo chanya

**RAIS** wa Indonesia, Joko Widodo, alifanya ziara ya siku mbili ya kiserikali nchini ambayo pamoja na mambo mengine, yeye na mwenyeji wake, Rais Samia Suluhu Hassan, walitiliana saini maeneo ya ushirikiano baina ya nchi zao.

Mikataba hiyo ya makubaliano inalenga kuyanufaisha mataifa hayo mawili pamoja na kudumisha uhusiano baina yao ulioanza mwaka 1965 na kutiwa saini na waliokuwa marais wa nchi hizo, Mwalimu Julius Nyerere wa Tanzania na Sukarno wa Indonesia.

Kwa kifupi ni kwamba baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulioanzisha taifa la Tanzania, ofisi ya kwanza ya ubalozi nje ya nchi ulifunguliwa nchini Indonesia, hali inayooonyesha kuwa nchi hizo zimekuwa na ushirikiano katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa muda mrefu.

Miongoni mwa maeneo ambayo viongozi hao walitiliana saini kwa ajili ya ushirikiano ni afya, nishati, madini, uchumi wa buluu, biashara, uwekezaji, viwanda na utalii. Katika kilimo, kwa mfano, Indonesia imeahidi kukifufua Kituo cha Mafunzo ya Kilimo kwa Wakulima Vijijini (FARTC) kilichoko Mkindo, Morogoro.

Katika afya, mathalani, kupitia mkataba huo, Tanzania inaweza kupeleka vijana kwenda kusomea fani za udaktari, uuguzi na famasia kutokana na Indonesia kuwa na vyuo vinavyotoa mafunzo kwenye ngazo mbalimbali za tiba na afya. Kwa maana hiyo Tanzania kupitia mkataba wa ushirikiano na kubadilishana uzoefu, inaweza kutumia nafasi hiyo kusomesha wataalamu wengi katika afya na hatimaye kupunguza kwa kiasi kikubwa pengo la wataalamu wa fani hizo.

Mbali na tiba, Indonesia imepiga hatua katika maendeleo ya sayansi na teknolojia ikiwamo kuwa na taasisi za elimu ya juu zinazofundisha kozi za ngazi mbalimballi katika eneo hilo ambalo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi. Eneo hilo pia Tanzania inaweza kutumia fursa hiyo kusomesha vijana wengi katika vyuo vya Indonesia kwenye masomo ya sayansi na teknolojia, uhandisi na kompyuta na hatimaye kuwa na rasilimali watu ya kutosha itakayochochea maendeleo ya taifa.

Aidha, kama inavyofahamika, nchi hiyo ni ya muungano wa visiwa mbalimbali ambavyo ni vivutio vikubwa vya utaliii na watu wengi duniani wamekuwa wakitembelea huko kwa ajili ya utalii. Tanzania pia ina vivutio mbalimbali vya utalii ukiwamo wa fukwe na visiwa kama Indinesia. Kutokana na mfanano huo, Tanzania inaweza kujifunza na kupata uzoefu namna marafiki hao walivyonufaika na sekta hiyo ambayo imekuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa pato la taifa.

Maeneo kama kilimo, viwanda na uwekezaji pia Tanzania inaweza kunufaika kwa kualika wawekezaji kutoka nchi hiyo ambao wamewekeza kwa kiwango kikubwa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo uongezaji thamani mazao ya biashara kama chai, mpira, kahawa na mkonge.

Tanzania kama ilivyo Indonesia, inazalisha mazao kama hayo pamoja na ya mafuta kama michikichi ambayo yameifanya nchi hiyo kuwa muuzaji wa biashara kama kahawa, chai na mafuta ya kupikia nje ya nchi na kuingiza fedha nyingi za kigeni na kuinua pato la taifa. Kupitia mkataba wa ushirikiano, Tanzania inaweza kunufaika kwa kualika wawekezaji wa viwanda vya kusindika mazao ya biashara yaliyoko nchini, hivyo kuongeza thamani, kuongeza ajira na kukuza uchumi wa nchi.

Ni dhahiri mkataba wa makubaliano kwa ajili ya ushirikiano katika maeneo mbalimbali yaliyoainishwa umefungua mlango mpya kwa manufaa wa kijamii na kiuchumi kwa Watanzania. Ni imani kwamba makubaliano hayo yatatekelezwa vyema kupitia sekta na taasisi husika na kuleta tija ya kweli.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Watanzania tudumishe utamaduni wetu, tuachane na zile za utandawazi

Na Tamary George

**KUTOKANA** na kukua kwa sayansi na teknolojia, moja ya vitu vinavochangia, ni uwapo wa utandawazi duniani.

Ikiwa utandawazi huo unasababishwa na uharibifu wa baadhi ya sanaa mbalimbali na tamaduni zetu za Kiafrika, kuna sanaa ambazo zinatambulisha nchi yetu ya Afrika .

"Utamaduni ni kiini cha roho ya taifa " alisema Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, akimaanisha kuwa nchi inapohusika na mkusanyiko wa watu, ni lazima kuwe na kiini cha roho na hapo ndipo kunakutwa utamaduni husika.

Bila ya hivyo, taifa linakosa uhai, kwani kiini cha roho kinakosekana. Wataalamu wametoa tafsiri ya utamaduni kuwa ni kielelezo cha mila, maisha na utashi wa jamii, kukiwapo ndani yake lugha sanaa na michezo ya jadi, pia mfumo wa maisha ya kila siku.

Kulingana na utamaduni na sanaa, vijana wanapata fursa nyingi za ajira kupitia utamaduni na sanaa walizo nazo mfano uchongaji wa vinyago, uchoraji, ubunifu wa mavazi, urembo kama vile pochi za namna mbalimbali, pia bangili, viatu, mikeka na picha. Zote hizo ni biashara kuu nchini Tanzania na mahali mbalimbali, kwani inaboresha utalii wa nchi katika sekta zote za kitaifa na kimataifa .

Joseph Christopher mkazi wa Mwenge Mpakani, Dar es Salaam, anayejisughulisha na kuchora, pia, kuchonga vinyago kwa kutumia rasilimali magogo ya miti, anasema "tunatakiwa kurudi katika utamaduni na sanaa zetu za kiafrika, ili kuepusha na kupunguza kasi ya utandawazi, kwani unaharibu utamaduni na sanaa zetu kutokana na mwingiliano"

**Msingi uliopo ni kwamba, sanaa hizo huwavutia watu wa mataifa mengine na wa ndani kwa ujumla, kwani huweza kutumika kama mapambo katika sehemu mbalimbali, mfano majumbani, ofisini na madukani.**

Pia, anasema watu wenye sanaa mbalimbali kama uchoraji, kuchonga, ubunifu wa mavazi ya asili na sanaa nyinginezo, wanaweza wakatumia ujuzi wao ili kuimarisha utamaduni na sanaa ya asili nchini, zikaimarika, kwani ujuzi huo unawaingizia watu vipato.

Msingi uliopo ni kwamba, sanaa hizo huwavutia watu wa mataifa mengine na wa ndani kwa ujumla, kwani huweza kutumika kama mapambo katika sehemu mbalimbali, mfano majumbani, ofisini na madukani .

Mkazi huyo anaendelea kutoa sababu za utandawazi namna unavyodidimiza utamaduni na sanaa ya nchini, akitoa mfano watoto na jamii kuchezea midoli inayotengenezwa kutoka viwandani, amabyo imekuwa changamoto dhidi ya kasi ya ukuaji wa utamduni wa asili nchini na Afrika.

Anamaliza Christopher kwa nafasi ya pekee, akimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi anayoifanya ya kuwaunga mkono wanaharakati wa kupigania utamaduni wa nchi, katika kuimarisha utamaduni katika njia ya kuitangaza katika matamasha mbalimbali ya asili.

Hapo ndipo anaitaja filamu aliyoitoa Rais aliyoshiriki kurekodi filamu ya Royal Tour, ambayo imetangaza utamaduni wa nchi, pia kulinadi taifa kitalii.

Anataja nafasi ya Rais Dk. Samia ameweza kuwahamasisha Watazania kuboresha utamaduni wao, kupitia filamu ambayo sasa iko kila mahali duniani, ikionyesha ufahari wa nchi yetu na utajiri iliyo nayo, hata kuwafanya vijana wengi wa kitanzania wameweza kuona ufahari wa utamaduni wa Afrika, maana hiyo ndio roho yake kuu.

# Mwanafunzi atoweka katika mazingira ya kutatanisha

**Na William Mngazija,** TANGA

MWANAFUNZI wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Mchanganyiko, Ilala jijini Dar es Salaam, Halima Khamara Haji (17) (pichani chini), anatafutwa na wazazi wake baada ya kupotea toka Juni tarehe 8, mwaka huu.

Mzazi wa mwanafunzi huyo, Khamara Haji, mkazi wa Kigamboni, ambaye alifika mkoani Tanga ili kumtafuta mtoto wake, alimwambia mwandishi wa habari hizi kuwa mwanawe alipotea tangu mwezi Juni na hajaripoti shuleni kwake.

Alisema ameripoti tukio hilo Kituo cha Polisi Mzizima, Kigamboni na kupewa kumbukumbu namba MZM/RB/304/2023.

Hata hivyo, alisema tangu aliporipoti tukio la kupotea mtoto wake, hajapatikana na kuliomba jeshi la polisi kuingilia kati kutokana na madai ya kuwapo tabia ya wanafunzi wa kike kupotea katika mazingira ya kutatanisha hatua ambayo imesababisha taharuki miongoni mwa jamii.

Alisema ni vyema jeshi la polisi likafanya uchunguzi kisha kuchukua hatua kwa baadhi ya watu wanaotorosha wanafunzi.

Alidai kuwa wapo baadhi ya wazazi wanaohusika kuwatorosha watoto wao kwa kushirikiana na baadhi ya watuhumiwa kwa sababu ya tamaa ya fedha.

"Wapo baadhi ya wazazi wanahusika katika zoezi la utoroshaji wanafunzi kwa sababu ya tamaa ya fedha, hivyo jeshi la polisi lifanye uchunguzi wa kina na kuwachukulia hatua kali za kisheria kwa sababu wanasitisha masomo kwa watoto wao," alisema.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Shule ya Sekondari mchanganyiko, Abeid Kamugisha, mwanafunzi huyo aliyesajiliwa shuleni hapo kwa namba **5669**, hajaripoti shuleni tangu mwezi Juni, mwaka huu.

Aliomba mtu yeyote atakayemuona mtoto wake apige simu namba **0782702222, 0743000061** au **0785978942**.





Aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), CPA Ludovick Utouh (kulia), akipatiwa huduma ya kujihakiki kwa kutumia simu janja kupitia App ya PSSSF kiganjani katika banda la PSSSF wakati wa kikao kazi cha wenyeviti na wakuu wa taasisi jijini Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madini ya shilingi bil. 9.2/- yaliyoibwa yakamatwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga limekamata vitu mbalimbali vya wizi yakiwamo mawe ya madini ya dhahabu yenye uzito wa gramu 6,753.4 yakiwa na thamani ya Sh. bilioni 9.2 yaliyoibwa katika machimbo ya dhahabu, Bulyanhulu.

Madini hayo yalikamatwa kufuatia msako uliofanywa na jeshi hilo kuanzia Julai 26 hadi Agosti 22, mwaka huu huku watuhumiwa wa wizi huo wakiendelea kusotoa rumande.

Akitoa taarifa ya kukamatwa kwa madini hayo jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alisema katika msako huo wamekamata vitu mbalimbali vya wizi, yakiwamo mawe yenye madini ya dhahabu yakiwa na thamani ya Sh. bilioni 9.2.

Vilevile, alitaja kukamatwa kwa 'carbon' yenye mchanga wa madini yadhaniwayo kuwa ni dhahabu yenye uzito wa kilo 261, katika maeneo ya Manzese, wilayani Kahama ambao mpaka sasa thamani yake haijajulikana.

"Madini haya tumeyakamata yakiwa yanatoroshwa ambayo yalikuwa yameibwa katika machimbo ya dhahabu Bulyanhulu na watuhumiwa tumewakamata wapo rumande," alisema Magomi.

Baadhi ya wadau wa madini mkoani Shinyanga wameiomba serikali kuweka ulinzi madhubuti katika maeneo mbalimbali ya uchimbaji ikiwa ni pamoja na kuacha kuamini kwa asilimia mia moja ulinzi wa kampuni binafsi.

"Katika awamu ya tano tuliona mbinu mbalimbali za kulinda utoroshwaji madini ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ukuta sambamba na kuweka ulinzi wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWT) hii itasaidia watu kuheshimu rasilimali za umma," alisema Estormine Henry, mfanyabiashara wa madini.

Aidha, alisema katika kudhibiti utoroshwaji wa madini upo umuhimu wa kuwekwa kwa sheria kali na kuzitekeleza ikiwa ni pamoja na watoroshaji wote wa madini kuondolewa dhamana kama ilivyo kwa makosa mengine ya jinai.

Katika hatua nyingine jeshi hilo lilitaja vitu vingine vya wizi vilivyokamatwa kuwa ni bunduki aina ya Riffle yenye namba 2/49PF78701 ambayo ilikuwa ikitumika katika shughuli za ulinzi bila kibali, bangi yenye uzito wa kilo 71, mafuta ya dizeli lita 603 yaliyoibwa katika mradi wa SGR, seti moja ya kompyuta, pikipiki tatu, boksi 14 za vigae na mabomba sita ya chuma.

Vitu vingine ni mabati 17, madumu matatu ya rangi, mifuko miwili ya saruji, saba ya chokaa, paketi 120 za vipodozi vyenye sumu na kukamata watuhumiwa 31 wanaouhusishwa na matukio ya wizi.

Katika hatua nyingine kamanda alisema wamekamata magari 3,084 kwa makosa mbalimbali ya usalama barabarani, ikiwamo kutokuwa na leseni, bima, mwendokasi, kuzidisha abiria, huku wakikamata madereva wa pikipiki 229 kwa kutovaa kofia ngumu, kuendesha pikipiki mbovu, madereva 64.

Alitaja idadi ya kesi zilizopata mafanikio mahakamani kwa makosa mbalimbali na kutolewa hukumu na wahusika kufungwa jela zikiwamo za ubakaji, ulawiti, kutorosha mwanafunzi, uvunjanji, kusafirisha dawa, kuharibu mali, pamoja na kukiuka masharti ya leseni ya biashara na mhusika alilipa faini Sh. 500,000.

Alitoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, kufuata sheria za nchi na kutoa ushirikiano kwa polisi taarifa za uhalifu ili kuendelea kudumisha amani ya nchi.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



# TAKUKURU yanasa nondo za chini ya kiwango mradi wa barabara

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma, imezuia tani 120 za nondo zisizokidhi viwango vya ubora kutumika katika ujenzi wa mradi wa barabara ya mzunguko wa nje jijini Dodoma.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, John Joseph, akitoa taarifa ya utekelezaji ya robo tatu ya mwaka, alisema jana jijini kuwa nondo hizo zilizotarajiwa kutumika katika ujenzi huo, zimekamatwa kwa ushirikiano wa TAKUKURU na Mkandarasi Mshauri na kuondolewa eneo la mradi.

"TAKUKURU Mkoa wa Dodoma ilifanya uchunguzi na kubaini nondo hizo hazina kiwango kinachostahili katika ujenzi wa barabara hii na kuamuru mkandarasi aagize nondo nyingine ambazo zina viwango vinavyotakiwa," alisema Joseph.

Vilevile, alibainisha kuwa taasisi hiyo imedhibiti wizi wa Sh. milioni 3.9 kutoka kwa mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ambazo ni za wanufaika wa Mfuko wa TASAF wa Kijiji cha Mlongia, wilayani huko. Zilitengwa kwa ajili ya wanufaika hao kukatiwa Bima ya Afya Iliyoboreshwa (iCHF).

"Mtumishi huyu alichukua fedha hizi kutoka kwa walengwa na kudai kuzipeleka kuwakatia bima, lakini hakufanya hivyo. Badala yake alikaa nazo mwaka mzima, akijinufaisha mwenyewe," alisema.

Alibainisha kuwa baada ya TAKUKURU kupata taarifa, ilifanya uchunguzi, mtumishi huyo amerejesha fedha katika akaunti namba 50510042226, ili zitumike kuwakatia bima ya afya ya walengwa hao.

Alisema TAKUKURU pia imekagua miradi 64 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 12.7. Miradi hiyo ni ya elimu, afya, ujenzi, maji na mifugo. Wameokoa Sh. milioni 41.2 ambazo zilikuwa katika hatari ya kufanyiwa ubadhirifu.

Mkuu huyo pia alisema walipokea malalamiko 54 yanayohusu rushwa na idara zinazolalamikiwa ni pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa - zinazoongoza, zikifuatwa na elimu, afya, ujenzi, madini, nishati, maji, umwagiliaji na mifugo.

Aliwataka watumishi wa taasisi hizo kujitathmini katika utendaji wao wa kila kila siku ili kukidhi mahitaji ya wananchi.

"Pia tunaendelea kufanya uchunguzi katika tuhuma zilizoainishwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na tuhuma nyingine kadri itakavyobainika, ili hatua stahiki zichukuliwe," alisema.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda (wa pili kushoto), akiangalia ramani ya ujenzi wa kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam eneo la Gongo, Kata ya Jamhuri mkoani Lindi jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walia kukosa majisafi miezi minne

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

NI miezi minne sasa tangu wakazi wa eneo la Shirika la Elimu Kibaha, Kata ya Tumbi, mkoani Pwani wakatiwe huduma ya majisafi kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA).

Kutokana na hali hiyo, wameomba mamlaka hiyo kuwarejeshea huduma hiyo ili waondokane na adha wanayokumbana nayo kwa sasa.

Cresencia Shirima, Balozi wa Kanda wa Shirika la Elimu Kibaha, alisema jana kuwa hawapati maji toka mamlaka hiyo tangu mwezi Aprili mwaka huu, hali inayosababisha kero kubwa.

Shirima alisema wamekuwa wakinunua sehemu nyingine. Dumu la lita 20 wanauziwa Sh. 500 na gharama ya kuyasafirisha, usafiri wa pikipiki ukitumika zaidi.

Optatus Katata, mkazi wa eneo hilo, alisema alipatiwa huduma ya maji mwaka jana, lakini maji yalikuwa yanawafikia mara chache hadi huduma hiyo ilipositishwa Aprili mwaka huu.

Imani Kayombo, alisema waliambiwa kero hiyo inatokana na msukumo wa maji kuwa mdogo, hivyo maji kushindwa kufika katika maeneo yao.

Kutokana na changamoto hiyo, Kayombo alisema hutumia gharama kubwa kupata maji.

Naye Mabuba Toksini, alisema imefikia hatua wanachukua maji sehemu wanazofanyia kazi, ingawa sasa wanategemea zaidi kununua maji yanayofikishwa mtaani kwa magari yanayouza maji mtaani.

Meneja wa DAWASA Kibaha, Alfa Ambokile, alisema changamoto hiyo inafanyiwa kazi kwa kuwa eneo hilo lina mradi na unaendelea kutekelezwa.

Ambokile, alisema mradi huo utakapokamilika, utaondoa changamoto hiyo kwa wakazi hao wa Tumbi na Mwanalugali. Huduma ya maji safi itarejeshwa.

# Kicheko soko la vinyago kuondolewa machinga

**Na Happy Peter**

WAFANYABIASHARA wa Soko la Kimataifa la Makonde Hand Craft Village, maarufu Mwenge Vinyago, wilayani Kinondoni, mkoani Dar es Salaam wamesema kuondolewa kwa machinga mbele ya maduka yao, kumerejesha wateja, wakiwamo watalii.

Wamesema kuwa awali machinga walikuwa wanafanya biashara mbele ya maduka yao na kusababisha wateja kukosa eneo la kuegesha magari yao.

Mwenyekiti wa Soko hilo, Khamis Juma, alisema kwa sasa wateja wao, wakiwamo watalii, ambao baadhi walikimbilia masoko mengine kutokana na kukosa maegesho, sasa wameanza kurejea.

"Kutokana na changamoto hii, niliandika barua kwenda kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kinondoni kuhusu kuwapo kwa machinga. Ni kero kubwa kwa watalii wanaofika hapa kununua vitu vya utamaduni. Walikuwa wanakosa eneo la maegesho ambalo machinga walilitumia kupanga chini bidhaa zao.

"Baadhi ya watalii ambao walikuwa wanakuja wakawa hawaji kwa kuhofia usalama wa mali zao. Baada ya serikali kuwaondoa (machinga) kwa sasa kuna ongezeko kubwa la watalii, tunaomba mchakato huu uwe endelevu kwa kuwa tuna familia na tunasomesha," alisema.

Juma alitaja kipindi wanachokitegemea kuwa na wateja wengi ni kuanzia mwezi Juni hadi Oktoba kila mwaka, hivyo kwa wakati huu, wateja wameendelea kuongezeka baada ya machinga kuondolewa.

Mfanyabiashara wa vinyago sokoni huko, Ally Juma, anayejitambulisha amefanya biashara hiyo kwa miaka 30, alisema kuondolewa machinga kumeleta faraja kwao kwa kuwa sasa wanapata wateja.

"Wateja wetu mara nyingi ni watalii na wapo wanaotoka ndani ya nchi. Wanapokuja na kukuta msongamano mbele ya maduka, wakati mwingine wanaona kama ni matapeli na mwisho wa siku wanasita kuingia sehemu zetu za biashara," alisema Juma.

Kulikuwa na idadi kubwa ya machinga katika eneo la Mwenge, lakini sasa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imechukua hatua ya kuwaondoa wafanyabiashara wadogo hao.

Nipashe imekuwa inashuhudiwa kuwapo magari ya Jeshi la Polisi na askari wa jeshi hilo wanaoshirikiana na askari wa Jeshi la Akiba (Mgambo) kuwadhibiti machinga kufanya biashara katika Soko la Mwenge.



## Asilimia 50 ya wanafunzi Babati wanaenda shule bila kula

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SERIKALI imekiri kuwa asilimia 50 ya wanafunzi wa shule za msingi katika Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, wanaathirika kitaaluma kutokana na kwenda shuleni bila kula kitu chochote asubuhi.

Kwa mujibu wa Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Mji wa Babati, anayeshughulukia lishe shuleni, Suzana Mushi, tatizo hilo limegundulika baada ya idara hiyo kufanya utafiti mdogo wa wanafunzi wa shule zilizoko katika mji huo.

Mushi, aliweka wazi tatizo hilo jana, mbele ya Ofisa Ustawi wa Jamii wa Mkoa wa Manyara, Khadija Muwango na menejimenti ya Shirika la COSITA waliohudhuria utambulisho wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali (PJT-MMMAM).

Ofisa huyo, alisema hata wanaokwenda shuleni wakiwa tayari wamekunywa chai, huwa ni chai ambayo haina kitafunwa, hivyo haiwasaidii kitu na wanaishia kupata udumavu. Alisema tatizo hilo, limesababisha watoto wengine kupata maradhi ya ugonjwa wa kisukari, kwa sababu ya kulishwa vyakula bila mpangilio.

"Kula Protini kila siku kunasababisha unene uliopitiliza, hivyo wazazi wasifikiri kula nyama kila siku ndio chakula bora,"alisema Mushi.

Mratibu wa PJT-MMMAM wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Martine Peter, alisema ni vizuri kuwa marafiki na watoto ili waweze kuwaambia wazazi vitu wanavyokutana navyo.

Akitoa elimu ya sayansi ya malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, Meneja Mradi wa Mtoto Kwanza kutoka Shirika la COSITA, Agustino Balohho, alisema wanasisitiza mtoto wa miaka sifuri mpaka nane kupata lishe ili imsaidie katika ukuaji wake na aweze kufikia utimilifu wake.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Abdulaman Kololi, alisema alifurahishwa na elimu iliyotolewa ambayo inawataka wazazi kujiandaa kabla ya kupana ujauzito na aliahidi kwenda kutoa elimu kwa wananchi.

# Matukio ya kupigwa wanaume K'njaro yawaibua wanaharakati

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MIGOGORO inayosababishwa na kuchipua kwa ukatili wa kiuchumi, ulawiti na vipigo dhidi ya wanaume katika Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, yameamsha hisia za makundi mbalimbali ya jamii na wanaharakati, wakiitaka serikali kuvunja ukimya na kushughulikia tatizo hilo kwa uzito zaidi.

Jana, baadhi ya wakazi wa wilaya hiyo waliozungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti kuhusu hali hiyo ambayo inatajwa kuvuruga taswira ya jamii iliyostaarabika kwa miaka mingi, imemwomba Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, kulitazama kundi la wanaume kwa jicho la tatu kutokana na kuathiriwa zaidi na ukatili.

"Tumesikia wanaume tayari wameanzisha dawati lao la kushughulikia matatizo yao ya ukatili wa kijinsia huko Jimbo la Vunjo, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, hilo peke yake linatosha kuonyesha kuna hali mbaya na kuna haja ya serikali na wadau wengine wa maendeleo kupiga kambi kukabiliana na hali hiyo," alisema Edward Mwendamseke, mtaalam wa saikolojia.

**Ili ukatili huo wa kiuchumi usiendelee katika maeneo mbalimbali nchini, ni vyema serikali ikaunda dawati maalum litakalofuatilia na kutatua malalamiko yanayowakabili wanaume wanaolia kusahaulika katika mambo mbalimbali.**

Mkuu wa Watawa wa Shirika la Dada Wadogo wa Mtakatifu Fransisco Tanzania, lililoko chini ya Kanisa Katoliki, Bridget Kokiambo, alisema kwa hali inayoendelea, iko haja kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Jeshi la Polisi, kuongeza ubunifu wa kukabiliana na ongezeko la vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanaume.

Aidha, mwanaharakati Victor Mbuya, alisema ili ukatili huo wa kiuchumi usiendelee katika maeneo mbalimbali nchini, ni vyema serikali ikaunda dawati maalum litakalofuatilia na kutatua malalamiko yanayowakabili wanaume wanaolia kusahaulika katika mambo mbalimbali.

Akizungumzia ukatili huo, Mratibu wa mradi wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya watoto na wanawake, Veronica Ollomi, alisema kwa sasa Shirika la KWIECO, kwa kushirikiana na Women Fund Tanzania Trust (WFT Trust), wameanza kuwapa elimu wanaume kuhusu ukatili huo kwenye Kata za Oldmoshi Magharibi, Kibosho Magharibi, Kirua Vunjo Kusini, Mwika Kaskazini na Mwika Kusini.

Kwa mujibu wa Veronica, mradi huo unalenga kuchangia uboreshaji wa msaada wa kisaikolojia, haki ya kielimu na kumaliza matatizo ya kiakili yanayohusiana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto mkoani Kilimanjaro.

Aidha, mradi huo unalenga kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake, wasichana na watoto kwa kuimarisha afya ya akili kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia, inayohusiana na ukatili kwa wanawake, wasichana, watoto na makundi mengine ya pembezoni na wale walioathiriwa na vikwazo vya unyanyasaji wa kitamaduni na mijadala katika jamii za vijijini na mijini.

Vilevile, unalenga kuhimiza haki za elimu kwa watoto wa kike kwa kuhakikisha kuwa vitendo vya ukatili wa kingono dhidi yao vinatokomezwa na jamii iwe mstari wa mbele kuhimiza na kusaidia wasichana kuingia tena katika mifumo rasmi ya shule.



Mtafiti kutoka Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), Prof. Stephen Maluka, akitoa mada kuhusu mabadiliko ya sekta ya afya, wakati wa mafunzo kuhusu uboreshaji wa huduma za afya kwa watendaji wa mitaa na wahudumu wa afya ya msingi ngazi ya jamii wilayani Handeni, mkoani Tanga, jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Mfumo wa hewa chanzo watoto wengi kuugua moyo

**Na Mary Mosha,** MOSHI

ASILIMIA 20 ya watoto waliofanyiwa uchunguzi wa kitabibu na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), kuhusu tatizo la moyo katika mikoa 11 nchini, kiini cha maradhi hayo kimegundulika kusababishwa na mfumo wa hewa.

Ripoti kuhusu uchunguzi huo uliofanyika mwaka wa fedha 2022/23 ilitolewa jana katika Hospitali ya Rufani Mawenzi Mkoa wa Kilimanjaro na Mkuu wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Upimaji wa Afya kwa Jamii, Dk. Padro Pallangyo.

Dk. Pallangyo, ambaye ni Daktari Bingwa wa JKCI, alisema uchunguzi wao umebaini kuwa katika asilimia 20 ya tatizo kusababishwa na mfumo wa hewa, mara nyingi chanzo ni mtoto kupata mafua na kutotibiwa kwa wakati na wengine hawasafishi vinywa vizuri.

"Kwa hiyo unakuta tatizo hilo linaanza kuruhusu kuzaliwa kwa bakteria na kuingia kwenye mfumo wa hewa, hivyo kuleta athari kwenye valvu za moyo.

...Kuhusu tiba, Dk. Pallangyo alisema: "Makundi yote mawili matibabu yake ni upasuaji. Huwa wanapogundulika wanapewa rufaa kwa ajili ya kupata matibabu ya kibingwa ya kurekebisha hizo valvu au kuziba hayo matundu.

Zaidi aliongeza: "Tukiachana na watoto, magonjwa mengine ambayo yameongoza kwenye kila eneo tulilokwenda, ni shinikizo la juu la damu ambapo kila kwenye watu 10, sita wanashinikizo la juu la damu, mengine ni moyo kupanuka na mishipa mikubwa ya damu kuziba. Wote hao wamepata rufaa ya kwenda kupata matibabu kwenye taasisi yetu."

Aidha, alisema umri unaoongoza ni miaka 45-65 kwa watu wazima na watoto kupata maradhi hayo, ni kuanzia mwezi mmoja hadi miaka 15, ingawa kumekuwa na ongezeko kubwa la shinikizo la juu la damu kwa vijana wenye umri wa miaka 18-35.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alisema katika Mkoa wa Kilimanjaro, jopo la madaktari bingwa linatarajia kuwafikia na kuwafanyia uchunguzi watu zaidi ya 1,500.

"Kwa siku mbili tu, tumewaona na kuwafanyia uchunguzi watu 600, wakiwamo watoto 60 wenye umri kati ya mwezi mmoja hadi miaka 15,"alisema.

Awali, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mawenzi, Dk. EdnaJoy Munisi, alisema Mkoa wa Kilimanjaro umeongeza matumaini makubwa ya uchunguzi huo, baada ya kuwapo kwa mwitikio mkubwa.

Alisema: "Uchunguzi huu utafanyika Mkoa wa Kilimanjaro, kwa siku tano, ukiwahusisha jopo la madaktari bingwa kutoka Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete.

Aliongeza: "Katika siku hizi mbili, uhitaji umekuwa mkubwa na bado kuna siku tatu zaidi mbele. Mawenzi tunategemea kupata watu wengi zaidi; na tutazungumza nao kuona uwezekano wa kurudi tena katika siku za hivi karibuni ili kuwasaidia wananchi wengine."



# Shilingi bilioni 19.5 kukarabati miundombinu Bandari ya Bukoba

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

SHILINGI bilioni 19.5 zinatarajiwa kutumika katika ujenzi wa miundombinu ya Bandari ya Bukoba mkoani Kagera.

Lengo la ujenzi na ukarabati wa bandari hiyo ni kuiwezesha kutoa huduma bora hususani itakapoanza kupokea meli ya mizigo ya Mv. Mwanza Hapa Kazi Tu.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Bandari hiyo, Marco Palanjo wakati akizungumza na Nipashe bandarini hapo na kueleza kuwa Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) liliangalia matatizo yaliyohitaji kufanyiwa kazi na kuona kuwa ipo haja ya kufanya upanuzi zaidi.

Alisema Bandari ya Bukoba ina maeneo finyu yanayolazimu kufanya upanuzi wa ujenzi mpya wa bandari, uboreshaji wa magati yaliyopo, upanuzi jengo la abiria, uchimbuaji na kuongeza kina cha maji, miundombinu ya umeme na maegesho ya magari.

**Lengo la shirika ni kuangalia utendaji wa maeneo ambayo yanathibitiwa na kuweka usalama wa vyombo vya majini na ufanisi katika bandari.**

"Bandari yetu kwa miaka mingi ilikuwa inafanyiwa maboresho madogo madogo lakini sasa tunafanya ujenzi na upanuzi ili watumiaji wa bandari wapate maeneo mapana kwa ajili ya ufanisi katika kazi," alisema Palanjo.

Alisema ujenzi na ukarabati huo tayari umeanza na sasa umefikia asilimia 13 na unatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi 18 na Julai 2024 utakuwa umekamilika.

Hata hivyo alieleza kupokea malalamiko ya mara kwa mara kutoka kwa watumiaji wa bandari hiyo juu ya kushindikana kuingia kwa meli kulingana na ufinyu wa eneo la kuegesha meli wakati wakisubilia mizigo na abilia wanaokwenda katika shughuli zao.

Mjumbe wa Bodi ya TASAC, King Shilagi alisema usalama wa vyombo vya majini unategemea utendaji wa shughuli za bandari na kuona kwamba usimamizi uliopo unafanywa kwa ufanisi.

"Lengo la shirika ni kuangalia utendaji wa maeneo ambayo yanathibitiwa na kuweka usalama wa vyombo vya majini na ufanisi katika bandari," alisema Shilagi.

Kadhalika, alieleza kuwa ili kufanya ushindani wenye usawa katika njia nyingine za usafiri yaliangaliwa matatizo ambayo yalikuwa ni kizuizi hali iliyofanya yawasilishwe serikalini.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, akionyesha kwa waandishi wa habari mkoani humo jana, jinsi watu walivyobuni mbinu za kuiba mafuta ya dizeli katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kwa kutumia chupa za maji. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Uzembe chanzo h'shauri kukusanya mapato kiduchu

**Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema iliyopo mkoani Mwanza, Yanga Makanga amesema uzembe wa wafanyakazi katika ofisi ya ukusanyaji mapato katika halmashauri hiyo kuwa ni chanzo cha kutofikiwa kwa malengo katika bajeti ya mwaka 2022/2023.

Aliyasema hayo juzi katika kikao cha baraza la madiwani cha robo ya nne na kusema kuwa ofisi hiyo haikusanyi mapato kama ambavyo inatakiwa na kuahidi kutokuendelea kuwavumilia watumishi wote ambao wanasababisha kushindwa kukusanya mapato kutokana na uzembe.

Mwenyekiti huyo alisema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 halmashauri ilikusanya Sh.milioni 374 sawa na asilimia 84 na kueleza kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 wanapaswa kukusanya kiwango lengwa ambacho ni Sh.milioni 400.

Alisema viongozi wote katika halmashauri hiyo kwa kushirikiana na watu wa idara husika wanatakiwa kusimamia kikamilifu upatikanaji wa mapato na kuhakikisha wanafikia malengo ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua wale wanaokwamisha shughuli hiyo.

Alitaja maeneo ambayo halmashauri hiyo inapoteza mapato kuwa ni pamoja na kwenye vivuko vya Kamanga, Busisi pamoja na Mkombozi kwa kushindwa kuvisimamia ipasavyo.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga aliitaka Ofisi ya Mkurugenzi ihakikishe inasimamia shughuli za ukusanyaji wa mapato katika halmashauri hivyo lengo likiwa ni kuiwezesha serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya kimaendeleo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Binuru Shekideli, aliahidi kuhakikisha anaendelea kusimamia ukusanyaji mapato ipasavyo na kufuatilia tatizo la wafanyakazi wazembe na kuwachukulia hatua stahiki.

Nao baadhi ya madiwani walisema viongozi hao wanatakiwa kusimamia vyema suala la mapato kwani ukusanyaji wa mapato ukiwa mzuri hata halmashauri inaweza kuwa na maendeleo na kujiendesha yenyewe.

Kwa mwaka wa fedha 2023/24 halmashauri hiyo inatarajia kukusanya zaidi ya Sh. bilioni mbili.

# Ukosefu wa vyoo waitesa Shule ya Sekondari Uzogore

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

DIWANI wa Ibadakuli Manispaa ya Shinyanga, Msabila Malale, amesema Shule ya Sekondari Uzogore inakabiliwa na uhaba mkubwa wa matundu ya choo, huku walimu wakiwa hawana sehemu ya kupata huduma ya choo.

Alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani Manispaa ya Shinyanga, wakati akiwasilisha taarifa ya kwenye kata yake.

Alisema kuwa shule hiyo ya sekondari ina matundu manne tu ya choo, huku walimu wakilazimika kujisaidia sehemu moja na wanafunzi.

"Hii ni moja kati ya kero kubwa katika kata yangu na inahitaji utatuzi wa haraka licha ya kuwepo na kero nyingine nyingi. Hii ni muhimu zaidi kufanyiwa kazi maana ni aibu na kushusha nidhamu na heshima ya walimu pale wanapotumia choo kimoja na wanafunzi wao,"alisema Malale.

Wakiwasilisha taarifa za kata zao katika kikao hicho, madiwani hao waliwasilisha kero ya upungufu wa matundu ya choo, walimu watendaji wa vijiji na mitaa na kuiomba serikali itatue adha hizo mapema.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Shinyanga, Saidi Kitinga, alieleza kuwa suala la walimu kuwa na choo chao ni muhimu na siyo kuchangia na wanafunzi.

Alisema serikali inapaswa kujenga choo ili kuwafanya walimu kuwa wa thamani ili wafanye shughuli zao za ufundishaji katika mazingira rafiki.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, alisema kero hizo zilizowasilishwa na madiwani zitashughulikiwa moja baada ya nyingine, kuwaomba madiwani wawe wavumilivu wakati serikali ikichukua hatua.

Aidha, Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Doris Dalia ambaye pia ni mwanasheria, alisema suala la utatuzi wa ukosefu wa matundu ya choo shuleni hasa Shule ya Uzogore litafanyiwa kazi haraka.

Hivyo aliwaomba wananchi washirikiane na serikali kutatua kero hiyo kwa kuchimba mashimo.

Kuhusu upungufu wa watumishi, alisema serikali bado inaendelea na juhudi za kupata watumishi wengine hasa watendaji ili kuziba nafasi zilizoachwa wazi.

**Serikali inapaswa kujenga choo ili kuwafanya walimu kuwa wa thamani ili wafanye shughuli zao za ufundishaji katika mazingira rafiki.**

# ama

**ALHAMISI AGOSTI 24, 2023**

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

## Prof. Kamuzora alivyozipa darasa bodi, kamati afya kufikia huduma



## Dk. Simwaza: Maradhi kinywa yana kila hatari kwa uhai wa mjamzito

Ukurasa 12

# Rais, Askofu Shoo wanavyobadilishana mawazo mazingira yanavyosimamiwa

**Na Peter Orwa**

JUMATATU wiki hii ina rekodi kubwa kwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), ikitimiza miaka 60 ya kuwapo kwake, tukio lililoendana na kikao cha ndani cha chombo hicho.

Pia, kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, naye akaangukia katika heshima kubwa kuwa mgeni rasmi wa tukio hilo la sasa, ikizingatiwa wakati chombo hicho kinaundwa, alikuwa katika umri wa miaka ya awali duniani.

Ni hafla iliyonakishiwa na ugeni wa aina nyingi, lakini katika upekee ni kuwapo wazee waasisi wa chombo hicho cha kiimani.

Katika hotuba yake, Rais Dk. Samia hakuficha ulivyo uhusiano wake na KKKT, mahususi akimtaja mkuu wake Dk. Fredrick Shoo anayempatia hadhi 'kaka yangu' kwamba wana utamaduni wa kuwasiliana kwa mashauriano ya kitaifa.

Awali katika hotuba yake ya kumkaribisha, Askofu Dk. Shoo akawasilisha wito wake kwa Rais Dk. Samia, akimkumbusha angalizo kwenye suala la usalama wa mazingira.

Katika namna ya kipekee kiongozi huyo wa kidini, kaielekeza mbali kwa maslahi ya vizazi vijavyo, akimuomba mkuu wa nchi akitumia mfano wa nishati mbadala kama makaa ya mawe, ikiwezekana kutumika nchini, ili kuitetea jamii ya Kitanzania.

Ni mada iliyomgusa Rais Dk. Samia, naye katika ufafanuzi wake wa hotuba, alipokabidhiwa kipaza sauti kuzungumza na umma, katika tukio hilo kubwa la KKKT linaloendana na mkutano wa siku kadhaa, akaja na majibu 'yaliyoshiba' kuhusu safari ambayo serikali imeshaanza kufanyia kazi kisekta, sheria na miradi yake.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akipokea tuzo kutoka kwa Askofu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Fredrick Shoo, kutambua jitihada zake za kuleta maendeleo nchini, Jumatatu wiki hii. **PICHA: MTANDAO.**

Kihistoria, Dk. Samia, ni mkongwe katika eneo hilo la mazingira, kwani katika zama za awamu ya nne ya uongozi wa nchi, alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Ni kipindi ambacho Rais wake, Dk. Jakaya Kikwete, kuna wakati akaongoza Kamati ya Mazingira ya Umoja wa Afrika (AU), ambayo ilishirikishwa katika hatua zote za kupatikana Mkataba wa Paris unaohusu mazingira duniani.

Huku Dk, Kikwete akiwa na historia ya mawasiliano ya moja kwa moja kuhusu mada hiyo kuelekea Mkataba wa Paris na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Ban Ki Moon, ikizingatiwa wawili hao wanafahamiana vyema tangu wakiwa mawaziri, ujumbe ukamfikia rasmi hata wakaunda ajenda ya Afrika, baada ya kutembelewa na mkuu huyo wa UN katika kikao cha AU nchini Guinea ya Equator, katikati ya mwaka 2015, Kamati ya Mazingira ya Afrika ikiwa chini ya Dk, Kikwete, ambayo ikateta naye.

Mchakato wake ukaanza rasmi nchini Marekani mwezi Septemba mwaka huo ma kisha ukapata baraka mwezi Desemba nchini Ufaransa, wakati, Dk. Samia kishapanda hadhi katika awamu ya tano, Makamu wa Rais mwenye mamlaka zaidi kwenye mazingira, endeleo lake la kuwajibikia kisekta.

Ilipofika Aprili 2016 mkataba wa Paris ulianza kufanya kazi ukiwa ndio mwongozo mkuu wa mazingira duniani unaotumika hadi sasa, ikimuacha Dk. Samia na mazingira ni sawa na 'kalamu na katarasi.'

### UFAFANUZI KWA KKKT

Kwanza, Rais Dk. Samia hafichi faraja yake katika uhalisia wana - kanisa anapowaona wanamuunga mkono katika juhudi za kukabili athari za mabadiliko ya hali ya nchi, akisema ni athari ya dunia nzima.

Huku akitumia nukuu za maandiko takatifu, pia wakuu wa kidini, Dk. Samia ananena "wanadamu wanakaidi maagizo ya Mungu...mazingira hayataacha kutuadhibu...'

Katika rai ya kanisa ikiomba kuharakishwa kwa mageuzi kuelekea nishati mbadala, Dk. Samia anasema serikali iko katika hatua za mbali kuwezesha matumizi ya kina ya nishati mbadala unaozalishwa nchini na kukabili athari za kimazingira nchini.

Pia, anataja lingine ni kuwapo mradi wa nishati ya upepo mkoani Singida, ikiwa sehemu ya mbinu mbadala katika kupata nishati.

Kimsingi, ni aina ya nishati ambayo wazo lake sio geni, lilishafanyiwa tafakuri za awali katika mkoa huo, katika zama za uongozi wa awamu ya nne nchini.

Rais Dk. Samia anasema ni hatua ambayo sasa inaendana na kujengwa mradi wa nishati jua mkoani Shinyanga, ambako nayo inaelekezwa kuongeza vyanzo vya nishati kitaifa.

Kwa mujibu wa Rais, katika mustakabali wa tabia nchi na usalama chakula, mradi wa uzalishaji chakula kwa kambi ya vijana mkoani Dodoma, unasonga kwa tija kubwa, wadau wa kimataifa wakiunga mkono, vyote vinaingia katika mjumuiko wa juhudi za kiserikali kuendana na hitaji la mbinu mbadala, dhidi ya mabadiliko ya mazingira na tabia nchi.

Rais akahitimisha kwa kutumia fursa hiyo kufafanua kwamba Tanzania inatarajia kuwa mwenyeji wa Mkutano Kimataifa wa Mfumo wa Chakula Kimataifa, kati ya tarehe 5 na 9 mwezi ujao, akialika mamlaka za kidini kushiriki ikiwa nayo sehemu ya kutekeleza ubia katika eneo la mazingira, kwa usirikiano kati ya mamlaka za umma na binafsi (PPP), inayosimamiwa na sera, pia sheria maalum iliyotungwa na uongozi awamu ya nne.

**Usikose kesho, safari ya PPP, uwekezaji na uzalishaji wa kesho nchini.**

AFYA

# Dk. Simwaza: Maradhi kinywa yana kila hatari kwa uhai wa mjamzito

## •Kwa mwanaume; kupooza, moyo, kansa…
## •Ukifungua mdomo; anajua ya leo, yajayo

**Na Beatrice Shayo**



AFYA ya kinywa na meno hasa kwa wajawazito, inatajwa isipozingatiwa, mtu anaweza kujifungua mtoto njiti.

Mtaalamu Dk. Katanta Simwanza, anaiambia Nipashe kwamba afya ya kinywa na meno, kila mtu anawajibika kuizingatia kwa usalama wa afya yake kwa jumla.

Anataja, mjamzito kinga yake inakuwa imepungua, hivyo hata mdomoni, afya yake inakuwa dhaifu, wadudu huzaliwa na kushambulia fizi.

"Baada ya kushambulia fizi hizo, fizi hutoa sumu ambayo ikiingia kwenye damu inakwenda kushambulia 'placenta' yaani mfuko ambao unamlea mtoto," anasema Dk Simwanza.

Anataja sababu ya watoto kuzaliwa njiti, ni mama anapokuwa na afya duni kinywani, pia asipozingatia usafi wake.

"Kuna vimelea vingine vikifika kwenye moyo vinasababisha kinamama wanapata kifafa cha ujauzito na wengine kupoteza maisha,"anasema Dk Simwanza.

Anaeleza changamoto nyingine ni meno kuoza na kwa wajawazito inakuwa tatizo kubwa, kwani inaweza kusababisha mimba kuharibika au kuzaliwa kabla ya siku zake.

"Kuoza kwa meno kunaweza kumsababishia mama kupata majipu na kupata changamoto nyingi na hatimaye kupata kifafa cha uzazi na hata kupoteza maisha yake,"anasema Dk Simwanza.

**KUBAINI SHIDA IJAYO**

Dk. Simwanza ambaye ni Mkurugezi Mwandamizi wa Taasisi ya Miracle Corners of World, Tanzania anaeeleza kitaalamu, daktari ana uwezo wa kukagua kinywa cha mtu akabaini changamoto ya miaka 20 ijayo.

Pia, anasema kinywa hutoa viashiria vya saratani ya tumbo. Anaendelea: "Daktari wa meno akiangalia meno yako anaweza kujua wakati unapatikana wazazi wako walikuwa na maambukizi ya... (maradhi) kutokana na meno yako yalivyokuwa."

Kwa mujibu wa Dk. Simmwanza, mtaalamu anamtambua kwenye hatari ya maradhi saratani, kisukari, shinikizo la damu, au maambukizi ya magonjwa yatokanayo na ngono, au kwa mtoto anayefanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Huku akisisitiza kinywa kina magonjwa mengi, anasema baadhi ya vitendo vinavyofanyika kwenye afya ya kinywa vinaweza kusababisha mtu akapata maambukizi ya vimelea akitoa mfano saratani ya shingo ya wa kizazi (HPV), pia saratani ya koromeo.

**UMUHIMU WA KINYWA, MENO**

Dk. Simwanza anasema, afya ya kinywa na meno ni eneo muhimu kuzingatiwa akihimiza: "Kinywa kinatuwezesha kula chakula na hata mmeng'enyo wa chakula inaanzia hapo. Kinywa pia kinatoa nafasi kinapokuwa salama watu kuwasiliana."

Anasema Umoja wa Mataifa (UN) kupitia Shirika la Afya Duniani (WHO) imetenga Machi 20 ya kila mwaka ni siku ya kuhimiza jamii duniani kuchukua hatua za kujikinga na kulinda afya ya kinywa na kwa miaka mitatu ikiwa na kaulimbii"jivunie kinywa chako, kithamini na kukitunza."

Anasema, kila mtu anashauriwa kuchunguza kinywa chake, pia taasisi na jamii zinahimizwa kuendelea kutoa elimu ya afya ya kinywa, huku matibabu yakitolewa katika vituo vya afya.

"Tunatakiwa kutambua katika masuala ya afya ya kinywa WHO alieleza daktari mmoja afya ya kinywa na meno anatakiwa kuwahudumia watu 75,000, kwa mwaka kwa Tanzania daktari mmoja anahudumia watu 125,000 kutokana na uhaba wa watumishi,"anasema.

**KOSA LA MSWAKI ASUBUHI**

Anasema kiafya inashauriwa mtu kupiga mswaki walau mara mbili kwa siku na kama ikiwezekana, mtu apige mswaki mara moja muda wa kwenda kulala.

"Kupiga mswaki asubuhi ni sawa na bure, kwa sababu wadudu wanakuwa wameshameng'enya chakula na kutoa sumu na kusababisha magonjwa ya kinywa,"anasema.

Anaeleza lengo la kupiga mswaki ni kuondoa masalia ya bakteria waliobaki mdomoni wasiyatumie kwa ajili ya kusababisha madhara, akifafanua bakteria wakiyatumia na kushiba, wanajisaidia na ndipo inakuwa sumu iliyolala mdomoni.

"Ukiona mtu ananuka mdomo sio kwamba mdomo unanuka. Mdomo unanuka vinyesi vya masalia yaliyosababishwa na hao bakteria wametoa kinyesi, mkojo, maji na takataka zote wanakuwa wameziweka pale mdomoni ndio maana utakuta mtu ananuka mdomo,"anasema Dk. Simwanza.

Anasema katika kuzuia meno kuoza wanahimizwa kupunguza ulaji wa vyakula na vinywaji vyenye sukari kila mara, pombe na matumizi ya sigara, kwani yana madhara makubwa kwa afya ya kinywa.

**KUEPUKA MARADHI**

Dk Simwanza anasema, ili kuepuka maradhi ya kinywa, watu wanapaswa kupiga mswaki walau mara mbili kwa siku.

"Meno yasitumike kama kifaa cha kufungulia vitu vingine, lakini wajitahidi kufanya uchunguzi wa kinywa walau mara mbili kwa mwaka,"anasema Dk Simwanza.

Anasema kwa mzazi au mlezi anatakiwa kuhakikisha mtoto anavyoota meno kuanzia miezi sita jino analisafisha kila mara na mtoto anapokuwa na umri kati ya miaka sita hadi tisa, anaanza kujifanyia usafi wa kinywa.

"Kuna baadhi ya kinamama wana tabia ya kumuacha mtoto amelala na nyonyo mdomoni ," anatamka na kuendelea: "Asilale akiwa analinyonya nyonyo anaweza kupata changamoto ya afya ya kinywa."

Anashauri kuna haja ya kuhakikisha kunakotolewa huduma za afya za jumla, suala la kinywa nalo liunganishwe, hata kuwezesha huduma ikiwafikia wengi, pia kupunguza usumbufu katika upatikanaji huduma hiyo.

Anawashauri kinamama wanapokuwa wajawazito, wahakikishe wanapata huduma ya afya ya kinywa na meno na hata baada ya kujifungua, ili kujilinda maambukizi ya magonjwa mbalimbali mdomoni.

Daktari huyo anataja stadi za kidaktari kuna wakati anaweza kuchunguza meno na kubaini rangi yake ilivyo, mara moja anapata majibu ya usalama wa mtoto katika nyumba anayoishi, ikiwamo wa ukatili wa kijinsia.

Anasema katika afya ya kinywa, baadhi ya wanaume wanaugua magonjwa ya kupooza viungo, mzizi wa tatizo ukiwa katika afya ya kinywa, moyo ukashambuliwa na kusababisha shida kwenye ubongo.

Daktari Simwanza anahitimisha kwa angalizo kitalaamu, kwamba afya ya kinywa na meno, badi imo katika kundi la magonjwa yasiyoambukiza, ambayo hayapati kipaumbele kikubwa.

> **"Tunatakiwa kutambua katika masuala ya afya ya kinywa WHO alieleza daktari mmoja afya ya kinywa na meno anatakiwa kuwahudumia watu 75,000, kwa mwaka kwa Tanzania daktari mmoja anahudumia watu 125,000 kutokana na uhaba...**

AFYA

## OFISA AFYA AFUNGUKA:

# Waumiza vichwa ushindani usio rasmi kinamama na ufahari watoto wengi

## • Mwenye wana 11, habari ya kawaida kifamilia

**Na Beatrice Moses, aliyekuwa Uvinza**

WAKATI kuna maeneo wanawake wanatumia dawa za uzazi wa mpango kudhibiti ujuazito usiotarajiwa, kuendana na uzazi wa mpango, katika baadhi ya maeneo wako kinyume na njia hizo kutaka kuwa idadi kubwa ya watoto, wakihisi ni ufahari, nyuma yake wakisukumwa na mila na tamaduni zao.

Hivi karibuni imeripotiwa na vyombo vya habari mnamo Agosti 18 mwaka huu, kwamba katika eneo la Mwika Kusini, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wanaume wanalalamikia kukithiri matumizi ya dawa za uzazi wa mpango, pia kunyimwa tendo la ndoa na wenza wao.

Inaelezwa kinamama wa maeneo hayo wanatumia sindano, vidonge, kitanzi na kutoshiriki unyumba, huku wanaume nao 'wamesusa' wametelekeza familia, pia hawashiriki kutunza familia ipasavyo, msuguano unaofanya wanawake nao kukazia msimamo wao, wakizama katika kujitafutia kipato.

Ni malalamiko yanayotajwa hadharani, Agosti 16, mwaka huu wakati wa mdahalo uliandaliwa na Shirika la KWIECO, kupitia Mradi wa Jitihada za Jamii kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya watoto na wanawake, unaofadhiliwa na Women Fund Tanzania Trust (WFT Trust).

Ni mdahalo uliohusisha wakazi wa kutoka vijiji vitano vya Kiruweni, Kimangaro, Mawanjeni, Kondeni na Matala vilivyoko Kata ya Mwika Kusini, waliokuwa wakijadili nguvu yao kupunguza au kutokomeza ukatili wa kijinsia na kuunga mkono shughuli za wanawake.

Hapo mkazi Bariki Kimaro anasema: "Unazungumza nini! sasa hivi watoto wako huku (anaonyesha kwa kupiga kwa mkono bega lake), nani ana muda wa kuzaa? Wanawake wanasema hawana muda wa kuzaa, wana muda wa kutafuta pesa,"

Grace Kihwelo, anarejesha hoja ya kujitetea kwamba wanaume wanakwepa majukumu ya kutunza wanawake wanapojifungua, pia hata hawawajibiki kulea mtoto kwa kumtimizia mahitaji yake muhimu, hali inayowafanya wanawake na wanajiongeza kwa kutumia ipasavyo njia za uzazi wa mpango ili wapate nafasi ya kujitafutia kipato chao, akikumbusha mtoto anakua na kuhitaji huduma kama malazi, elimu,




Hafla ya kukabidhi msaada wa magodoro na vitanda katika Hospitali ya Mkoa wa Kigoma.

**KILICHOKO KIGOMA**

Mnamo Juni mwaka huu, mwandishi wa makala hii akiwa mkoani Kigoma, alipata ufafanuzi wa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Dk. Boniface Manditi na Ofisa Afya wa Wilaya ya Uvinza, Hussen Katelanya, kuhusu kinachojiri katika eneo lao.

Ofisa Afya, Katelanya anaiambia Nipashe kuwa baadhi ya wanawake wa maeneo hayo wanakwamishwa mikakati ya uzazi wa mpango, kwa vigezi vya Imani za kidini, tamaduni na hulka ya kushindana kwa kutaka kujigamba kuwa na watoto wengi.

Katelanya anasema, licha ya uzazi wa mpango kulenga uimarishaji wa afya zao na watoto, pia wanaume, bado wanapinga dhana hiyo inayowapa fursa kujihusisha zaidi kiuchumi.

"Wao wanaona kuzuia, yaani kuchelewesha kuzaa ni kinyume na amri ya Mungu . Pia, familia ikiwa na idadi ya watoto wachache, inadharaulika kwa kuwa inajenga taswira kuwa hata ukoo wao ni mdogo," anasema.

Ofisa Afya anadokeza kuwapo mashindano yasiyo rasmi ya kuzaa, ili kufanikisha idadi kubwa ya watoto, akitoa takwimu ni kawaida kumpata mama mwenye idadi ya watoto kufika 11.

Katelenya anasema, kinyume chake huwa wanakwama katika uwezo kuwalea ipasavyo, wakishindwa kumudu gharama za malezi bora, hivyo wanadorora kiafya, kutokana na lishe duni.

"Wana tabia ya kujadili idadi ya watoto kwa kuangalia familia, angalia fulani ana watoto wawili yule anao watatu, wanachekwa licha ya kwamba ukifuatilia familia zenye watoto wachache, wana afya bora kwa kuwa wazazi wanamudu malezi ya kuwapa chakula bora," anasema.

**MGANGA MKUU**

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Dk. Manditi, anabainisha suala la uelewa kuhusu afya kwa wakazi wa maeneo hayo upo, ikiwamo linalohusu lishe bora, chanjo na uzazi wa mpango.

Dk. Manditi anasema, licha ya changamoto kama umbali na hali duni ya miundombinu katika badhi ya maeneo, wamekuwa wakijitahidi kutoa huduma ya afya kwa wananchi.

Dk. Manditi anasema kuna hospitali moja katika wilaya hiyo, vituo vitano vya afya na zahanati 38, hivyo kwa magonjwa yanayowakabili wakazi wengi wa willaya hiyo homa ya matumbo, mkojo mchafu (UTI) na minyoo, ikichangiwa kwa kiasi kikubwa na tabia ya kula udongo kwa baadhi ya watoto na wajawazito.



Moja ya zahanati katika hatua ya ujenzi wilayani, Uvinza, mkoani Kigoma. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Anataja changamoto ya utoaji huduma ya afya, pia inachangiwa na miundombinu kuharibiwa na mvua, pia umbali wa kufika kwenye maeneo hayo akitoa mfano kitongoji cha Ubanda Kata ya Karia.

"Kuna wananchi kadhaa wanaishi huko, lakini ili kuwafikia unalazimika kupita Mpanda mkoani Katavi, ndipo uweze kufika. Huko hakuna zahanati, lakini wanapaswa kupata huduma ya afya ikiwamo chanjo muhimu kwa watoto,"anasema .

Ubovu wa barabara unawagharimu wagonjwa wakati wa masika kukodi usafiri wa pikipiki unaowagharimu hadi Sh. 200,000 ili kufuata huduma ya matibabu iliko.

Anasema, kuna huduma ya zahanati ya kuwahudumia Ukanda wa Ziwa Tanganyika, wanaokwenda kuhudumia vituo vya huko waliko.

Anatumia nafasi hiyo kutoa wito kwa wadau wa afya kuona umuhimu wa kujenga zahanati.

**UTAFITI ULIVYO**

Ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi uliofanyika Kigoma, mwaka 2014 na Kituo cha Kudhibiti Magonjwa nchini Marekani (CDC), inaonyesha matumizi ya uzazi wa kati ya asilimia 79 waliotolewa wahatumii njia yoyote, wakati asilimia tisa wanatumia sindano na asilimia saba, wanatumia njia nyingine za kisasa za uzazi wa mpango na asilimia tano, wanatumia njia za asili za uzazi wa mpango.

Imebainishwa kuwa asilimia 45 wana mtazamo ya kuwa familia ni lazima ziwe na watoto wengi, kwani wengine wanaweza kufa, wakati asilimia 74ya wanawake wa Kigoma walipata ushauri nasaha kuhusu uzazi wa mpango wakati tayari wakiwa wajawazito.

Katika utafiti huo, ufanisi na usalama wa vichocheo vya kuzuia mimba unaonyesha wanawake wengi wa Kigoma hawafahamu kuwa njia za kisasa za uzazi wa mpango ni salama zaidi.

**MRATIBU MKOA**

Mnamo April 21 mwaka huu, Mratibu wa Huduma hiyo kimkoa Bernadetha Peter, akiwasilisha taarifa ya hali ya viashiria vya Huduma ya Afya ya Uzazi Mama na Watoto kwa Mkoa wa Kigoma, akiwa kwenye uzinduzi wa Mpango wa "M-mama" kwa Mkoa wa Kigoma kupunguza vifo vya wajawazito, waliojifungua na watoto nchini, anasema sababu mojawapo ni kukosekana elimu ya afya na Huduma ya Uzazi miongoni mwa wanajamii.

Pia, anataka , uhaba wa wataalam wenye weledi katika kutoa huduma hiyo kwa wakati.

Anasema, idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi ambapo kwa mwaka 2018 vifo vilikuwa 78, 2029 vifo 100, 2020 vifo 119, 2021 vifo 75 na Mwaka 2022 Jumla ya vifo ilikuwa 102

AFYA

# Prof. Kamuzora alivyozipa darasa bodi, kamati afya kufikia huduma



Viongozi wa juu wa serikali, walipokagua Kituo cha Afya cha Sunya katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, kilipokuwa kikijengwa.
**PICHA: MTANDAO.**

**Na Christina Mwakangale, aliyekuwa MBARALI**

NAPOZUNGUMZIWA huduma za afya ngazi ya vituo, zahanati na hospitali kuhusu ubora wake na changamoto, kuna mamlaka za wananchi zinazohakikisha zinaboreshwa, ikiwamo upatikanaji dawa, vifaa tiba na miundombinu.

Hiyo ni majukumu ya bodi na kamati za usimamizi wa vituo vya afya vya halmashauri, zinazopokea na kuchambua mipango na bajeti ya kituo cha afya, taarifa za fedha za robo mwaka kubuni vyanzo vipya vya mapato, hata kuidhinisha matumizi.

Mfumo wa bodi na kamati za utendaji, zinataka kuwa za ushirikiano na wadau wa sekta ya afya kwenye halmashauri, lengo ni kuboresha huduma.

Kuwapo kwa bodi na kamati zinazosimamia utendaji kwenye vituo na sekta ya afya ni wa kisheria, chimbuko lake liko katika Sheria za Serikali za Mitaa Mwaka 1999, inayoshusha madaraka ya serikali kuu hadi ngazi ya vijiji na mitaa.

Profesa Peter Kamuzora, kutoka Taasisi ya Taaluma za Maendeleo (IDS) ya Chuo Kikuu Dar es alaam (UDSM), anafafanua chimbuko la mabadiliko hayo kwa sekta ya afya nchini, wajumbe, wenyeviti, makatibu wa bodi na kamati hizo, pia maofisa na watendaji kata.

Msomi huyo anafafanua hayo katika mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi na Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Afya, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, yaliyoandaliwa na Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) na makao makuu UDSM na kufanyika wilayani hapa.

Anasema yanalenga kundi mahsusi katika wilaya za Mbarali, Mbeya na Handeni, Tanga. Hiyo ni baada ya utafiti kubaini kamati na bodi hizo, wajumbe wake na wananchi hawana ufahamu sahihi wa majukumu na umuhimu wa nafasi zao

Mtaalamu huyo anarejea katiba ya nchi inavyoeleza umuhimu wa kuundwa kwa serikali za mitaa katika wilaya na miji, katika katiba, akisema:"Ibara ya 146 inazungumzia madhumuni ya serikali za mitaa katika kukasimu madaraka kwa umma. Ndivyo kamati na bodi hizi zinachokifanya zimekasimishwa madaraka, ili kuutumikia umma."

Pia, anataja malengo ya kutekeleza mabadiliko ya serikali kuruhusu halmashauri kuunda sheria ndogo za kuboresha utendaji kazi, akisema mabadiliko katika sekta ya afya nchini tangu uhuru, 1961, ni sehemu ya mabadiliko ya jumla katika nyanja za uchumi, huduma za jamii na mgawanyo wa madaraka.

"Mabadiliko katika sekta ya afya yalianza mwaka 1994. Mabadiliko haya hasa yanalenga kuboresha hali ya afya na ustawi wa Watanzania, ni mabadiliko ya msingi katika sera, sheria, miongozo na mfumo mzima wa utoaji wa huduma za afya nchini, ili kuboresha hali ya afya ya mwananchi," alisema Profesa Kamuzora.

Analalamika kushuka ubora wa huduma kunakoendeleza hali duni ya afya kwa umma, huku watu wakiongezeka ikilinganishwa na uwezo wa serikali katika sekta za afya.

Mwanazuoni huyo anataja mambo kama uhaba wa rasilimali za kuboreshea huduma za afya kama vile dawa, majengo, vitendea kazi, watumishi wenye ujuzi, ni sababu ya mamlaka ya usimamizi kushushwa kwa umma.

Pia, anasema ushirikishwaji mdogo wa jamii katika masuala yanayohusu afya zao, kupungua ari ya kazi miongoni mwa watumishi, ushiriki mdogo wa sekta binafsi na wadau wengine, kunashinikiza hitaji la maboresho ya sekta hiyo.

Anaendelea: "Kuongeza ushiriki wa jamii katika kuchangia gharama za huduma za afya; kuboresha utendaji na kuondoa kero za wananchi katika upatikanaji wa huduma za afya; kuhakikisha uwapo wa dhana ya uwajibikaji na ushirikishwaji wa jamii katika utoaji wa huduma za afya na kuhakikisha huduma bora zinawafikia wananchi wote bila kujali hali ya kipato."

### MABADILIKO SEKTA AFYA

Profesa Kamuzora anasema, serikali imesogeza madaraka karibu na wananchi kupitia halmashauri zao kuboresha huduma za afya, upanuzi wa huduma na usimamizi wake.

Anataja ni mabadiliko yenye manufaa, huku Wizara ya Afya ikizingatiwa kutoa huduma, kutunga sera na sheria, kuweka viwango vya huduma, kutafuta rasilimali na kufuatilia huduma zake kwa wananchi.

"Matokeo na maendeleo katika utekelezaji wa Mabadiliko katika Sekta ya Afya nchini, baadhi ya hatua za mabadiliko zilizofikiwa hadi sasa ni kuanzishwa Mipango Kabambe ya Mwaka ya Huduma za Afya kwa kila halmashauri nchini (CCHP); Mpango Kabambe wa Vituo vya kutolea Huduma za Afya (Hospitali, Kituo cha Afya na Zahanati). Kuanzishwa kwa Bodi za Afya za Halmashauri na Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Afya," anafafanua

### MATOKEO YA MABADILIKO

Profesa Kamuzora anasema mabadiliko kwenye sekta ya afya imewezesha wananchi kushirikishwa katika mipango ya afya ya mwaka, pia kuamua katika huduma za afya kupitia wawakilishi wao kwenye Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Afya ngazi ya Zahanati, Kituo cha Afya na Hospitali na Bodi za Huduma za Afya za Halmashauri.

"Serikali imeongeza uwezo wa vituo vya afya na zahanati kwa kupanga, kusimamia na kumiliki huduma zinazotolewa kutumia rasilimali za vituo, zikiwamo fedha (vituo vinamiliki fedha baada ya kuruhusiwa kufungua akaunti benki).

"Matokeo na maendeleo katika utekelezaji wa Mabadiliko katika sekta ya afya nchini kwa upande wa Wizara ya Afya, inaendelea kushughulikia uanzishwaji wa bima ya afya kwa wananchi wote, inaendelea kushirikisha sekta binafsi na wadau wote katika kuimarisha huduma za afya," anafafanua.

Anaongeza: "Serikali imezifanyia sheria mapitio na kuanzisha nyingine: Kwa mfano: Sheria ya Bima ya Afya ya Taifa (mwaka 1999) na Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii (mwaka 2001), imebuni vyanzo vingine vya mapato kugharamia huduma za afya (papo kwa papo), Bima ya Afya, Mfuko wa Afya ya Jamii."

### BODI NA KAMATI

Mwanasheria wa Halmashauri ya Mbarali, Herman Mpogole, anasema Bodi za Afya za Halmashauri zipo kisheria kutekeleza utawala wa sheria wa kukasimu madaraka kwa wananchi na serikali yao.

Pia, Mpogole anasema ni namna shirikishi katika uwajibikaji wa wananchi kusimamia huduma za afya na kujenga uwezo wao kumiliki huduma za afya zinazotolewa na vituo vyao.

Anasema halmashauri kupitia Sheria ya Serikali za Mitaa, inapata mamlaka ya kuunda bodi katika halmashauri husika.

"Bodi hizi zitawajibika katika halmashauri na zitatekeleza kazi zake kama ambavyo itaainishwa katika hati rasmi. Hati hiyo itaainisha kipindi cha bodi kuwa madarakani, uhusiano na jamii wadau mbalimbali, sifa za wajumbe," anaeleza mwanasheria huyo.

Wilayani, anataja vyombo vya aina tatu, Bodi ya Afya ya Halmashauri, Timu ya Uendeshaji Afya ya Halmashauri; na Kamati ya Usimamizi wa Hospitali.

Ni bodi inayotajwa kuwajibika kupitia Kamati ya Huduma za Jamii, uwajibikaji anaoutaja kujumuisha dhana ya umiliki, uwezo wa kuajiri, kufukuza au kuondoa, pamoja na kusimika au kuvunja bodi.

### UWAJIBIKAJI KWA JAMII

Mpogole anasema bodi itawajibika kwa jamii katika kusimamia utoaji huduma bora za afya katika halmashauri husika, kuhakikisha kunakuwapo mfumo wa kutoa taarifa na mrejesho kati ya bodi na kamati za vituo.

"Kuhakikisha uwepo wa uhusiano mzuri kati ya watoa huduma na watumia huduma. Wajumbe wote wa kuchaguliwa, watawajibika kwa waliowachagua kwa kukusanya maoni kabla ya kikao na kutoa mrejesho baada ya kikao, wale watakaoshindwa kutimiza wajibu huu wabadilishwe mara moja.

"Mjumbe yeyote wa kuchaguliwa atakayekosa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo, atapoteza nafasi ya ujumbe na abadilishwe mara moja, kwa kufuata taratibu za kisheria," anafafanua Mpogole.

Mpogole anasema bodi ina wajibu na mamlaka kamili ya utawala na uendeshaji huduma za afya kwenye halmashauri husika.

Pia, inatakiwa kuwa na uhusiano wa kiutendaji na Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Huduma, Mpogole akifafanua: "Bodi haitakiwi kuingilia masuala ya kitaalamu ya watumishi mradi wapo katika mipaka ya maadili ya kazi. Kama mjumbe wa Bodi analazimika kujiuzulu anatakiwa kutoa notisi ya mwezi mmoja kwa Katibu wa Bodi."



## Mtendaji wa Kijiji, mkusanya mapato watupwa mahabusu

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali, ameamuru kukamatwa Mtendaji wa Kijiji cha Iguguno, Kiraka Monge pamoja na mkusanya mapato wa kijiji hicho, Manase Kizula, kwa kosa la kukusanya ushuru kutoka kwa wananchi bila kuwapa stakabadhi za malipo.

Machali alitoa agizo hilo juzi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kijijini hapo kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi wa Kata ya Iguguno.

Katika mkutano huo, wananchi wa kijiji hicho walimweleza mkuu huyo kuwa wajasiriamali wadogo wamekuwa wakilipa ushuru wa bidhaa tangu mwaka 2019 lakini hawajawahi kupewa stakabadhi na wakusanya ushuru, jambo linalowatia wasiwasi huenda fedha hizo zinaishia mifukoni.

Baada ya malalamiko hayo ya wananchi, Machali alimwita Mtendaji na mkusanya ushuru kutoa maelezo lakini walishindwa kujieleza na hivyo kuamuru Jeshi la Polisi liwasweke ndani.

Aidha, Machali alimuagiza Ofisa Utumishi Wilaya ya Mkalama kushughulikia watendaji wote wanaokiuka maadili ya utumishi wa umma.

"Katika kipindi nitakachokuwa Mkalama nitahakikisha napambana na wabadhirifu wote ili kila mtumishi aweze kutenda haki kwa wananchi wakati wa kutoa huduma," alisema.

Pia, alimtaka Kaimu Mtendaji wa Kata ya Iguguno, Paul Grindai, kuhakikisha anaanzisha mchakato wa kupata Baraza la Ardhi la Kata baada ya lile lililokuwepo awali kuvunjwa kutokana na kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Alisema: "Utoe tangazo kwenye mbao za matangazo ili wananchi wenye sifa za kuwa wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kata kugombea nafasi hizo ili kuhakikisha migogoro ya ardhi inaanza kutatuliwa ngazi ya kata kabla ya kwenda ngazi ya wilaya".

# Waajiri, wahitimu kujadili fursa soko la ajira nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) imeandaa kongamano la ajira linalolenga kuwakutanisha wahitimu wa Programu ya Kukuza Ajira na Ujuzi kwa Maendeleo Afrika (E4D) pamoja na waajiri ili kushirikishana fursa za soko la ajira.

Kaimu Mkurugenzi wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Abdallah Ngodu, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kongamano hilo linaloandaliwa na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ) litakalofanyika leo jijini hapa.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi sita za Afrika zinazotekeleza mradi huo unaofadhiliwa na wizara ya Shirikisho la Ujerumani la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo(BMZ) na Shirika la Ushirikiano la Maendeleo la Korea (KOICA), unaolenga kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa vijana 4,000 na hadi sasa 3,258 wamenufaika.

Alibainisha kuwa vijana hao wamenufaika katika vyuo vya VETA vya Dodoma, Manyara, Lindi, Singida, Mikumi, Gorowa na Dakawa kupitia fani za ufundi bomba wa majumbani, viwandani, uchomeleaji vyuma viwandani na mekatroniki.

**Mradi huo ulilenga kuwaanda vijana kupata ajira kwenye uwekezaji unaofanyika hapa nchini na kujiajiri ili kupata kipato kilicho halali.**

"Inatarajiwa nguvukazi yenye ujuzi kutokana na mradi wa E4D itatumika katika kukuza ajira kwenye miradi ya kimkakati ya uwekezaji kama vile bomba la mafuta, Bwawa la Nyerere na treni ya mwendokasi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2023," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema katika kongamano hilo kutakuwa na maonyesho ambayo yamelenga kujenga uelewa juu ya fursa za ufundi stadi zilizopo kwenye mradi na kukuza uwezo wa kuajirika kwa wanufaika wa kozi zinazotolewa na vyuo vya VETA chini ya mradi wa E4DT.

Pia, alisema wahitimu wataonesha umahiri wa ujuzi wao katika bidhaa walizotengeneza na miradi wanayotekeleza.

"Utekelezaji wa mradi wa E4D unagusa viwanda ambapo mpaka sasa viwanda na kampuni zaidi ya 20 zimethibitisha kushiriki na zitaonesha huduma na bidhaa zao, tunaamini kampuni pia zitapata fursa muhimu ya kuthibitishiwa kwa uhalisi kuhusu umahiri na ujuzi wa wahitimu wa mafunzo ya ufundi stadi ili wajenge imani na hatimaye kuwapatia fursa za ajira vijana hao," alisema.

Kadhalika, alisema kwenye kongamno hilo pia kutakuwa na taasisi za fedha ambazo zitatoa fursa za uwezeshwaji hususani mikopo inayoweza kuwanufaisha vijana waliopata ujuzi ili wawe na mitaji ya kuendesha shughuli za uzalishaji na kuongeza vipato na ajira endelevu.

Naye, Mshauri wa Ufundi, Leah Dotto, alisema mradi huo ulilenga kuwaanda vijana kupata ajira kwenye uwekezaji unaofanyika hapa nchini na kujiajiri ili kupata kipato kilicho halali.




Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Mkoa wa Dodoma, John Joseph, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu kukamata nondo zisizo na kiwango cha ubora, ambazo zilipangwa kutumiwa katika ujenzi wa mradi wa barabara ya mzunguko wa nje inayojengwa katika eneo la Nala-Veyula-Ihumwa Bandari Kavu mkoani humo. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# TOSCI: Tumieni mbegu zenye ubora ili kuongeza mavuno

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) imewataka wakulima kuacha matumizi holela ya mbegu na badala yake watumie ambazo zimethibitishwa ubora ili kuongeza mavuno, tija na kipato.

Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Patrick Ngwediagi, alisema hayo juzi jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo na mwelekeo wa mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema ili kilimo kiwe na tija nchini wakulima wanapaswa kutumia mbegu zenye ubora na zilizothibitishwa na taasisi hiyo ili kuongeza mavuno na kipato.

"Wito wangu kwa wakulima na jamii kwa ujumla tumieni mbegu zilizothibitishwa ubora ili kuongeza mavuno, tija na kipato badala ya kuendelea kutumia mbegu ambazo hazina ubora na kupunguza tija kwenye kilimo nchini"alisema

Akizungumzia kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24, alisema watatumia Sh.bilioni 12.6 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali ikiwamo kuendelea na uboreshaji wa shughuli za utafiti na usimamizi wa ubora wa mbegu.

"Taasisi itaendelea kuboresha shughuli za uthibiti na usimamizi wa ubora wa mbegu zilizoanzishwa katika mwaka wa fedha uliopita katika maeneo mbalimbali,"alisema.

Kadhalika, alisema shughuli nyingine ni kutekeleza mradi wa kuendeleza sekta ya kilimo na uvuvi kwa kujenga maabara yenye uwezo mkubwa itakayofanya kazi ya uchambuzi wa mambo mbalimbali yanayohusu mbegu katika makao makuu ya TOSCI.

Aidha, alisema pia wamepanga kujenga maabara ya mbegu kwenye tawi la taasisi hiyo Kanda ya Ziwa mkoani Mwanza, kuandaa na kutekeleza mkakati wa kuelimisha umma juu ya matumizi ya mbegu zilizothibitishwa ubora za zenye lebo ya TOSCI, kuthibitisha na kusimamia ubora wa miche/vipando na pingili za mazao ya miti ya matunda, migomba na miwa.

Hata hivyo, alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita taasisi hiyo imesajili zaidi ya mbegu 647 na kuwachukulia hatua watu wote waliobainika kuuza mbegu feki kwa kuwafikisha mahakamani.





# Kibano madereva ‘STK’ wanaovunja sheria

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi limetangaza kuanza kuwashughulikia madereva wa magari ya serikali na mashirika ya umma wanaokiuka sheria za usalama barabarani, ili kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea na kusababisha madhara kutokana na uzembe.

**Mabasi yaliyopewa kusafirisha abiria usiku yanatakiwa kusimamiwa kwa ukaribu ili kuhakikisha abiria wanaoyatumia wanamaliza safari zao salama.**

Mkuu wa Ufuatiliaji na Tathimini wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Naibu Kamishna wa Polisi Fraiser Kashai, aliyasema hayo alipofanya ziara ya kikazi mkoani Mbeya kwa lengo la kufuatilia hali ya utendaji kazi wa wadau wa usalama barabarani.

Akizungumza kwenye kikao cha wadau, Naibu Kamishna Kashai, alisema madereva wa magari ya serikali wanatakiwa kuwa vinara wa kufuata sheria za usalama barabarani ili madereva wa magari mengine wajifunze kutoka kwao.

Aliwaagiza wakuu wa vikosi vya usalama barabarani nchini kote kuwachukulia hatua za kisheria madereva hao kwa maelezo kuwa sheria hazibagui madereva wa serikali wala wa magari binafsi.

“Hawa wana leseni kama walivyo madereva wengine, kwahiyo wachukulieni hatua za kisheria ikiwemo kuwatoza faini, dereva wa magari ya serikali anapokiuka sheria za usalama barabarani ni kosa kubwa sana,” alisema Kashai.

Awali Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani ya Mkoa wa Mbeya, Rajabu Ghuriku, alisema madereva wa magari ya serikali wamekuwa wakikiuka sheria na taratibu wanapoendesha magari hayo kutokana na kuwaendesha viongozi.

Alisema madereva hao wamekuwa wakigoma kusimama wanapoamuriwa na askari wa usalama barabarani jambo ambalo limekuwa likiwapa wakati mgumu katika kuzuia ajali za barabarani.

Alisema tatizo hilo limekuwa kubwa hasa kwenye maeneo ya miteremko mikali ambayo Kamati ya Usalama Barabarani ya mkoa kwa kushirikiana na viongozi wa serikali katika mkoa huo walianzisha utaratibu wa magari makubwa na madogo kupita kwa awamu.

“Hawa madereva huwa wanajiona kama vile wanakuwa wamebeba serikali nzima, wakisimamishwa hawasimami sasa tunaomba mtusaidie ili tukomeshe tatizo hili maana madereva wengine huwa wanajisikia vibaya wanapoona sheria zinang’ata upande mmoja,” alisema Ghuriku.


Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ramadhani Ng’anzi, aliagiza askari wa usalama barabarani waongezwe ili kuimarisha ukaguzi wa magari yanayopita.

Aidha aliagiza elimu ya usalama barabarani kuongezeka pamoja na kuongeza vipimo vya ulevi kwenye vizuizi ili kuwadhibiti madereva ambao wamekuwa wakitumia pombe na dawa zingine za kulevya wakati wakiendesha magari.

Aidha, alisema mabasi yaliyopewa kusafirisha abiria usiku yanatakiwa kusimamiwa kwa ukaribu ili kuhakikisha abiria wanaoyatumia wanamaliza safari zao salama.

Naye Mjumbe wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, Naibu Kamishna Mstaafu wa Jeshi la Polisi, Mohamed Mpinga, alishauri yafanyike makongamano mbalimbali yenye lengo la kutoa elimu kwa watumiaji mbalimbali wa barabara kuhusu usalama.

Alisema elimu ni muhimu kuliko njia zingine zinazochukuliwa zikiwemo za kisheria na hivyo akalitaka Jeshi la Polisi kutumia njia mbalimbali kutoa elimu ikiwemo matumizi ya vyombo vya Habari.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako (kulia), akisikiliza maelezo kutoka kwa kijana mwenye ulemavu, Moses Nkubi (kushoto), kuhusu teknolojia mbalimbali zinazobuniwa na wanafunzi wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST), alipofanya ziara ya kikazi chuoni hapo jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wachangishana fedha kujenga maabara ya kijiji

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

WAKAZI wa Kijiji cha Ilininda wilayani Ludewa Mkoa wa Njombe, wamechangishana shilingi milioni sita ili kuanza ujenzi na ununuzi wa vifaa vya maabara ya kijiji.

Baadhi ya wananchi hao wamesema adha imekuwa kubwa hususani katika upande wa maabara kwa sababu wataalamu wa afya wamekuwa wakibashiri ugonjwa kwa sababu hakuna maabara.

Wamesema kutokana na changamoto hiyo wakazi wa kijiji hicho wameamua kuchangishana fedha kwa kushirikiana na wadau wengine ili kuwaondolea adha hiyo sambamba na kuepuka ramli chonganishi ambazo zimekuwa chanzo cha migogoro na mauaji.

Ditrick Mlelwa, alisema kuwa katika kijiji chao hakuna maabara yeyote hata ya binafsi hali inayosababisha kupata shida.

“Mara wagonjwa wanapojitokeza manesi wetu wamekua wakifanya matibabu kwa kukisia kwa kuangalia dalili”alisema Mlelwa.

Naye, Teodosya Msanga alisema wamekuwa wakitumia dawa ambazo siyo sahihi kutokana na ugonjwa ambao wanakuwa nao.

“Kwa sababu unafika tu hospitali unakuta mtu anabuni kwamba unaumwa hiki hana uhakika anakupa tu dawa ambazo hazina uhakika lakini kupitia michango hii tunaamini sasa tunakwenda kupata tiba sahihi”alisema Teodosya.

Hata hivyo Lawi Mnyanga, aliiomba serikali kuwashika mkono ili kuongeza nguvu ili kukamilisha ujenzi maabara na ununuzi wa vifaa tiba.

“Tunaiomba serikali ituunge mkono kwenye hili baadhi ya vifaa ambavyo sisi tutashindwa kwa sababu kuna vifaa vya maabara vingine vinakuwa na gharama kubwa serikali inaweza ikatusaidia”alisema Lawi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ilininda, Exavel Mlelwa, alisema ili kupata vipimo wanalazimika kwenda mbali na kijiji chao.

“Tunalazimika kwenda Ikelu Makambako ni mbali sana lakini sasa hivi tunaona itakuwa ni jambo jema sana,” alisema Mlelwa.

Mwenyekiti wa Shirika la Kuhamasisha Maendeleo kwa Wananchi (ECF), Johnson Mgimba, alisema waliibua wazo ambalo liliungwa mkono na wananchi na kuanza kuchangishana ili kutatua changamoto hiyo.

## Maonyesho Nanenane yawakuna wanafunzi Sekondari Sangu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHULE ya Sekondari Sangu iliyopo jijini Mbeya imeipongeza serikali na wadau mbalimbali walioshiriki katika Maonyesho ya Wakulima ya Nanenane yaliyofanyika hivi karibuni, wakisema yalikuwa na mambo mengi ya kujifunza hasa kwa vijana.

Wanafunzi wa kidato cha tano katika shule hiyo waliyasema hayo juzi walipozungumza na waandishi wa habari waliotembelea shule hiyo kwa lengo la kupata tathimini ya vijana kuhusu kujiajiri kwenye sekta ya kilimo.

Walisema miongoni mwa mambo yaliyokuwa muhimu kujifunza ni pamoja na uwepo wa nyenzo za teknolojia za kisasa za kilimo ambazo zinavutia vijana kujiingiza kwenye sekta hiyo.

Mmoja wa wanafunzi hao, Oscar Mwakyusa alisema wanaanza kuvutiwa na ajira ya sekta ya kilimo kutokana na teknolojia iliyopo hivi sasa kuonesha njia sahihi ya kuwakwamua vijana kutokana na uwepo wa zana za kisasa.

Vilevile alisema serikali imeweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo pamoja na uhakika wa masoko kwa ajili ya masoko ya mazao ya wakulima.

Naye Hussein Mwaipopo, alisema teknolojia pia ya kuongezea mazao thamani inaonekana kurahisishwa kwa sasa tofauti na iliyozoeleka, ilikuwa na gharama kubwa hata kusababisha wadau wa kilimo wasio na mitaji mikubwa kushindwa kuimudu.





# Chanzo utoro wanafunzi Kijiji cha Kigongoni chatajwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UELEWA mdogo wa umuhimu wa elimu kwa wakazi wa Kijiji cha Kigongoni Mkoa wa Kaskazini Unguja umesababisha tatizo la utoro kwa wanafunzi wa Shule ya Maandalizi na Msingi ya Kidagoni mkoani humo.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Machano Khamis Machano, alibainisha hayo na kusema wanafunzi wengi shuleni hapo huishia porini na kushindwa kufika shule kupata elimu.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari waliofanya ziara kijijini hapo kwa lengo la kuwasikiliza wananchi kutokana na changamoto zinazowakabili zipatiwe ufumbuzi.

Ziara ya waandishi wa habari iliandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA, Zanzibar).

Mwalimu Mkuu huyo alisema wanafunzi hao bado ni wadogo, wanahaki ya kupata elimu lakini hawafiki shuleni licha ya kuondoka nyumbani kwao kwa lengo la kwenda shule lakini huishia kujificha porini.

Alisema wanafunzi hao wanakosa haki yao ya msingi ya kupata elimu kutokana na changamoto nyingi za kijamii ikiwemo kutembea umbali mrefu wa kwenda na kurudi shule.

**Yapo matukio mawili ambayo tumeyapata shuleni hapa ya wanafunzi yanayoashiria kutaka kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji wakati wanapokuja na kurudi shule, wakiwa huko njiani hukutana na wahalifu ambao hawana nia njem.**

"Shule yetu inatumiwa na wanakijiji wa majimbo manne na kama shule unavyoiona ipo mbali na makazi ya wanakijiji na imezungukwa na pori, hivyo kwa mtoto mdogo wa maandalizi na msingi ni vigumu kutembea bila ya uwangalizi kutoka nyumbani kwao hadi kufika shuleni"alisema.

Aidha, alisema wastani kwa siku hukosa wanafunzi 35 kwa darasa moja ambao hawafiki shule na kukosa masomo hali ambayo inarejesha nyuma maendeleo yao kielimu.

Pia alisema mikakati wanayoifanya katika kupunguza tatizo hilo la utoro wanatoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa elimu na kuwafuata na kuwasaka wanafunzi wanaoishia porini.

Hata hivyo alisema ipo haja ya kujengwa kwa shule nyingine ya maandalizi na msingi katika moja ya vijiji vilivyopo katika eneo la Kigongoni ili kuwapunguzia wanafunzi changamoto ya kutembea umbali mrefu.

Alisema kitendo cha watoto kutembea masafa marefu kutafuta elimu pia ni hatari kwao kwa sababu kuna hatari ya kukutana na vitendo vya udhalilishaji.

"Yapo matukio mawili ambayo tumeyapata shuleni hapa ya wanafunzi yanayoashiria kutaka kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji wakati wanapokuja na kurudi shule, wakiwa huko njiani hukutana na wahalifu ambao hawana nia njema," alisema.

Baadhi ya wanafunzi waliozungumza na waandishi wa habari walisema kutembea umbali marefu Kwenda shule ni tatizo kwao kwa sababu hakuna usafiri wa gari utakaowawezesha kufika shuleni.

Khairati Haji ni miongoni mwa wanafunzi wa shule hiyo, alisema licha ya kutembea umbali mrefu kwenda na kurudi shuleni lakini mazingira anayopita ni hatarishi.

Sheha wa Kigongoni, Vuai Mtoshubure, alisema shehia yake imezungukwa na vijiji 11 ambavyo vipo mbali na huduma ya elimu, hivyo huwalazimu watoto kutembea umbali mrefu wa zaidi ya kilomita mbili kutafuta elimu.



Wanafunzi wa Shule ya Maandalizi Kidagoni, Mkoa wa Kaskazini Unguja wakiwa darasani shuleni hapo, jana. Wanafunzi hao, hulazimika kutembea umbali mrefu wa zaidi ya kilomita mbili kufuata elimu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mhadhiri chuo kikuu ahimiza upatikanaji haki za binadamu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), Profesa Mohammed Awadelkarim, amesema haki za binadamu zinapaswa kutolewa, kulindwa na kutimizwa pasipo kuwapo na ubaguzi.

Alisema kutekeleza misingi ya haki za binadamu ni jambo lisilo na mipaka ambalo linapaswa kupewa umuhimu na kila nchi duniani kwa kuhakikisha hakuna mtu anayenyimwa haki zake.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua warsha ya mafunzo kwa watetezi wa haki za binadamu, wadau wa msaada wa kisheria na wanafunzi wa fani hiyo.

Profesa Mohammed alisema suala hilo la haki pia limetiliwa mkazo na dini zote duniani.

Alisema hakuna dini hata moja inayopinga binadamu kutendewa haki na kwamba zinawafundisha waumini kutenda mema na kuepuka kudhuriana ili kujenga mahusiano mazuri kwao.

Aidha, alisema haki za binadamu ni kitu adhimu na tunu katika nchi yoyote na vigumu kuwa na uhuru kamili kama haki hizo hazipewi thamani inayostahili.

Alisema pamoja na umuhimu wa uhuru kwa kila binadamu, hakuna mwenye haki ya kuvuka mipaka na kuzivunja haki za mwingine hata kama amekosewa, kwamba zipo njia za kushughulikia kisheria ili kuleta suluhu badala ya kuendelea kuvunja haki.

Kadhalika, alisifu jitihada za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Mapinduzi Zanzibar, kwa kuhakikisha zinatekeleza maazimio ya jumuiya za kimataifa yanayohimiza haki za binadamu, utawala wa sheria na demokrasia.

Naye, Mratibu wa Mtandao wa Utetezi Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Ole Ngurumwa alisema kwa mujibu wa azimio la Umoja wa Mataifa la Mwaka 1948, nchi inaposaini maazimio inalazimika kuheshimu, kulinda na kuzitimiza haki za binadamu.

Alisema Umoja wa Mataifa (UN) ulifikia hatua ya kuweka azimio hilo baada ya kuona haki mbalimbali za binadamu zikivunjwa kutokana na matukio na hujuma nyingi zilizosababishwa na vita kati ya nchi, migogoro ya kijamii, kisiasa, kidini na mengine.

Hata hivyo, alisema ili kuhakikisha kila binadamu anatimiziwa haki zake za msingi, serikali zote na vyombo vya kusimamia haki hizo zinawajibika kutathmini utendaji wao ili kujiepusha na matendo yanayosababisha kuzikiuka.

# Serikali yabariki juhudi za wawekezaji uzalishaji sukari

**Na Mwandishi Wetu,** Zanzibar

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema inaunga mkono jitihada zinazofanywa na wawekezaji katika kusaidia uzalishaji na upatikanaji wa sukari ambayo inazalishwa nchini.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban alipokutana na uongozi wa Kiwanda cha Sukari Mahonda kilichopo Wilaya ya Kaskazini B Unguja alipofanya ziara iliyolenga kuona uzalishaji katika kiwanda hicho.

Alisema, vitendo vinavyofanywa na baadhi ya wananchi kuchoma moto mashamba ya miwa ni uhujumu uchumi na husababisha hasara kubwa kwa uzalishaji wa sukari.

Aidha, aliwataka wananchi hao waache tabia hiyo, kwamba serikali haitamvumilia mtu yoyote atakayefanya vitendo hivyo na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Aidha, alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kusaidia juhudi za uzalishaji kwa kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo hayo ili kuepusha kutokea kwa vitendo hivyo.

Akifafanua kuhusu mauzo ya sukari, alisema serikali bado haijaruhusu bidhaa hiyo kuuzwa nje ya nchi, hivyo wafanyabiashara wahakikishe wanauza bidhaa hiyo ndani ya Zanzibar na kwa bei halali iliyowekwa na serikali.

Meneja Rasilimali Watu wa kiwanda hicho, Bashir Waziri Mohammed, aliishukuru serikali na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa jitihada wanazozichukua kwa kuwaunga mkono na kushirikiana katika kuweka mipango mikakati ya uzalishaji wa sukari nchini.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

FOMU MIRATHI – 2
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya Temeke
Kituo cha Jumuishi Mkoa Dar es Salaam
Usimamiz wa mirathi Na 1231/2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU Seif Abdallah Liumu
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA
NA Abadallah Seif Liyumu

TANGAZO
(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 14 Mwezi 09 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia ;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetolewa leo Tarehe 22 Mwezi 08 Mwaka 2023

HAKIMU

---

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
WILAYA YA KINONDONI
MWANANYAMALA
SHAURI LA MADAI NAMBARI 509 LA 2022
MELANIA EMILIO MOYO......MWOMBAJI/ WAOMBAJI
(1)GABRIEL ALEX (2) MOHAMED MANINGA
(3) KALISTO RAPHAEL (4) KALENGA MAFTAH (5)
SAKUBU MUSSA................MDAIWA/WADAIWA
WITO KUITWA SHAURINI
(1)GABRIEL ALEX (2) MOHAMED MANINGA
(3) KALISTO RAPHAEL (4) KALENGA MAFTAH
(5) SAKUBU MUSSA

**POPOTE ULIPO/MLIPO**
MELANIA EMILIO MOYO amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni ( Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa hukumu tarehe 5/9/2023 saa 3.00 Asubuhi mbele ya Mh. J.W.SILLAS vielelzo vyote vya kesi vinapatikana katika masijala ya wazi Baraza la Ardhi na Nyumba Kinondoni. Endapo hautatekeleza haya, Shauri litasikilizwa upande mmoja na Hukumu kutolewa.
Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 09 Mwezi 08 ....2023

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MUSTAPHA MOSHI RUMEZE** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya TVS STAR yenye usajili namba: MC 239 DBP na CHASSIS NAMBA: MD625AF41M1F13439. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**DAR/URA/RB/267367/2023**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MBEYA
KITUO CHA MJINI..............MKOA WA MBEYA
SHAURI LA MADAI/NDOA Na 79/2023
Jina la mdai PILLY JUMA LISSU
Jina la Mdaiwa FADHIL KAPANGE
KUITWA SHAURINI MDAIWA
Kanuni ya 18 ya kanuni ya utaratibu wa madai katika Mahakama za Mwanzo

**Kwa; FADHIL KAPANGE**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba[Eleza hapa habari za madai] NI JUU YA MAOMBI YA KAKAZA HUKUMU.Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 4 mwezi wa 9 mwaka 2023 saa 08;30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta mashaidi/shaihidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO;Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 21 mwezi wa 8 mwaka 2023

HAKIMU


---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**MOHAMED THABITI IMAMU** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji aina ya TVS KING yenye usajili namba: MC 493 CLY na CHASSIS NAMBA: MD6M14PAXL4AL9580. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:**
**SOG/RB/3269/2023**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACKLINE PATRICK TETI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S5097-0022 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia SHULE YA SEKONDARI ALCP KILASARA mwaka 2017. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/KIL/MOS/21/2023**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**REGISTERED OF THE ARCHDIOCESE OF DAR ES SALAAM** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **ISUZU** yenye usajili namba: **T 695 ACQ, CHASSIS NAMBA: UBS169EW711220** na **ENGINE NAMBA: 4JGZ2773613.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi taarifa:
**PHQ/DAR/KIN/867/2023**

---

## TANGAZO LA MNADA

Work ethic Company Limited Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Magari jijini Dar es salaam Mteja anashauriwa kulipa deni ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | Mahali dhamana ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Hussein Ramadhani Daphy | TOYOTA HARRIER T896 ASA | 08.09.2023 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa Mawasiliano piga 0713801904 ( Work ethic) au 0677014355(Fanikiwa).**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GOODCHANCE ANDARSON KISANGA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 313 CZN . Chasses Namba DD51T589561, Engine Namba F6A6813788. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Polisi Taarifa :
**KIL/MOS/RB/154627/2023**

---

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MOSHI.
WILAYA YA MOSHI
MAOMBI NA. 88/2023
SCOLASTIKA HERMAN ASSENGA............MLETA MAOMBI
DHIDI YA
FRIDA HERMAN ASSENGA ................MJIBU MAOMBI NA.1
FERDINAND HERMAN ASSENGA......MJIBU MAOMBI NA.2
MASABA NEHEMIA MASABA............MJIBU MAOMBI NA.3
KUITWA SHAURINI

**KWA FERDINAND HERMAN ASSENGA**
Kwa kuwa mleta maombi ameleta madai ya kesi na yameelezwa katika nakala ya madai ambayo inapatikana katika Baraza la Ardhi na Nyumba Moshi. Shauri limepangwa kutwajwa tarehe 14/09/2023 saa bili na nusu (2:30)asubuhi mbele ya Mheshimiwa Mwenyekiti H. LUKEHA hivyo unatakiwa kufika mahakamani wewe au wakili wako.
ANGALIA: Kama hautahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu Mahakama itasikiliza shauri hili na kutoa uamuzi upande mmoja.
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 15 mwezi Agosti,2023

...... ...

---

IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
TEMEKE SUB-REGISTRY
(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)
AT TEMEKE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 68/2023
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MICHAEL NYARI YONA
AND
IN THE MATTER OF PETITION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY LILIAN GODFREY KAMUKALA
CITATION WHERE CONSENT IS NOT AVAILABLE
(Rule 72(2))

**To: THELESIA PETER PAKATA**
**WHEREAS, LILIAN GODFREY KAMUKALA** of Dar es Salaam has petitioned to this court for letters of administration of the estate of Michael Nyari Yona, decease.
**AND WHEREAS**, it has been disclosed to this court that you have an interest in the estate of the said deceased.
**YOU ARE HEREBY CITED** to come and see the proceeding if you think fit before the grant is made.
Objections to the grant should be filed on or before the 25th day of September, 2023.
**Dated at Dar es Salaam this 22nd day of August, 2023**

DEPUTY REGISTRAR

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALLY SAID MANJAVILA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SUZUKI VITARA GOLD yenye usajili namba: T 765 DKV na CHASSIS NAMBA: JSAJTDA4V00140686. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:**
**SO/RB/5024/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BENJAMIN BENJAMIN MJOMBE** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya SANLG S125 yenye usajili namba: MC 242 BBQ na CHASSIS NAMBA: LBRSP-JB52A9054525. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:**
**SO/TR/RB/4218/2023**

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
Probate and Administration Cause No 98 of 2023
In the Matter of the Estate of the late
PETER JUSTINE KULAMIAWA of miganga within Dodoma region
AND
In the matter of application for letters of administration by ESTER JULIUS MAKALI AND JOHN JUSTINE PAUL
GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 13 day of 09...........2023
Dated at Dodoma this 23 day 08.............2023

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATHEW JOHN MHAGAMA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya MITSUBISH FUSO yenye usajili namba: T862 AFR na CHASSIS NAMBA: FK417J542767. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:**
**SO/RB/7901/2019**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**CECILIA JULIUS MOGORE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0233-0014 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia ST. MARY'S MAZINDE JUU SECONDARY SCHOOL mwaka 2017. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/3757/2023**

---

KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA
SHAURI LA MAOMBI LA ARDHI NA. 85 YA 2022
JOHN SOLOMON DAGARAZA ........................ MLETA MAOMBI
DHIDI YA
MACHONJE JOSEPH KIMOSA NA MWENZAKE ..... WAJIBU MAOMBI

**KWA:** MACHONJE JOSEPH KIMOSA.
**POPOTE ULIPO.**

**KUITWA SHAURINI.**
Unaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya tarehe **15/9/2023** siku ya **Ijumaa** saa **3:00 asubuhi** ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.

**Eleweni kwamba**, ukikosa kufika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo hii, tarehe **2/8/2023**.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATHEW JOHN MHAGAMA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya ISUZU yenye usajili namba: T952 AVK na CHASSIS NAMBA: JALHTR11-JN3000225. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:**
**SO/RB/7900/2019**

---

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku
Piga Simu 0677020701

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
**THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wazimbabwe wapiga kura

**HARARE, Zimbabwe**

RAIA wa Zimbabwe wamejitokeza katika vituo vya kupigia kura jana kukamilisha muda wa miezi mitatu ya kampeni ya kuwania nafasi ya uchaguzi wa urais, ubunge na udiwani.

Wananchi hao walianza kujitokeza alfajiri katika vituo vya upigaji kura katika maeneo mbalimbali nchini humo.

Serikali ilitangaza jana kuwa siku ya mapumziko ili kuwaruhusu wapigakura milioni 6.62 waliojiandikisha katika daftari la kudumu.

Rais Emmerson Mnangagwa, anawania nafasi huyo huku wagombea wengine 10 akishindana nao.

Mgombea ambaye anaonekana kuwa mpinzani wake wa karibu ni Nelson Chamisa kutoka chama kikuu cha upinzani cha Citizens Coalition for Change (CCC).

Ili kushinda kiti cha urais mpya, mgombea anatakiwa kupata zaidi ya asilimia 50 ya kura.

Ikiwa hakuna mshindi wa moja kwa moja, uchaguzi wa pili ya urais itafanyika baada ya wiki sita.

Uchaguzi huo ni wa kwanza tangu kifo cha rais wa kwanza wa taifa hilo Robert Mugabe, ambaye alitawala siasa za nchi hiyo na chama tawala cha Zanu-PF kwa miongo kadhaa.

Alifariki miaka miwili iliyopita baada ya kuondolewa madarakani katika mapinduzi ya kijeshi na nafasi yake kuchukuliwa na naibu wake Mnangagwa.

Vituo vya kupigia kura vilifunguliwa saa moja asubuhi na kuwaruhusu wapiga kura waliowahi vituoni kupiga kura kwa kuwachagua viongozi hao.

Kabla ya siku ya kupiga kura, maafisa wa uchaguzi walikuwa wakiandaa vituo vya kupigia kura katika mji mkuu, Harare, na kuondoa mabango ya kisiasa ambayo yangeharibu sheria za uchaguzi.

Polisi wamesambazwa nchini kote ili kudumisha hali ya amani na utulivu.

Kulingana na mkuu wa polisi nchini humo, Godwin Matanga, idadi yao imeongezwa na askari magereza katika kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika kwa amani.

**BBC**



Wananchi wa Zimbabwe wamejipanga kwa ajili ya kuingia katika vyumba vya kupigia kura jana jijini Harare.
**PICHA: REUTERS**

# Sudan yazidi kuteketea

**KHARTOUM, Sudan**

MAPIGANO makali yanaendelea kuzunguka kambi ya kimkakati ya jeshi katika mji mkuu wa Sudan, Khartoum wakati Jeshi la Sudan (SAF) na Kikosi cha Dharura (RSF) wakipambana.

Katika taarifa yake iliyochapishwa kwenye ukurasa wake wa Facebook jana usiku jeshi lilisema kwamba lilizuia shambulio jingine la wapiganaji wa RSF kwenye kambi yake katika eneo la Al-Shajara, kusini mwa Khartoum na kusababisha hasara kwa jeshi la wanamgambo.

Kwa upande wake, RSF ilidai kuchukua udhibiti wa sehemu za kambi na kukamata silaha nyingi.

Katika taarifa yake iliyochapishwa kwenye mtandao wa kijamii wa X, ambao zamani ulijulikana kama Twitter ilisema kambi hiyo wameidhibiti.

Tovuti ya televisheni ya Al Arabiya inayofadhiliwa na Saudia iliripoti kuwa jeshi bado lilikuwa linadhibiti kambi hiyo baada ya siku tatu za mapigano makali.

Mapigano kati ya vikosi hivyo viwili yamezidi kuongezeka katika siku za hivi karibuni katika mji mkuu Khartoum na miji ya jirani ya Omdurman na Bahri pamoja na sehemu za eneo la magharibi mwa Darfur.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, maelfu ya watu wameuawa na wengine zaidi ya milioni nne wamekimbia makazi yao tangu mzozo huo kuzuka katikati ya mwezi Aprili.

**BBC**

## Ethiopia kuchunguza mauaji

**ADDIS ABABA**

SERIKALI ya Ethiopia imesema itaichunguza ripoti ya shirika la kutetea haki za binaadamu la Human Rights Watch kuhusu mauaji ya mamia ya raia wake katika mpaka wa Yemen na Saudi Arabia.

Wizara ya Mambo ya Kigeni ya Ethiopia ilisema uchunguzi huo utafanywa kwa ushirikiano na maafisa wa Saudia.

Human Rights Watch yenye makao yake mjini New York ilitoa ripoti yake Jumatatu ya wiki hii, ikieleza simulizi za mashuhuda wa mashambulizi yaliyofanywa na walinzi wa mpakani nchini Saudi Arabia wakitumia bunduki za rashasha na maguruneti dhidi ya Waethiopia ambao hawakuwa na silaha waliojaribu kuingia katika taifa hilo la Kifalme kutokea Yemen.

Wizara hiyo ilitoa wito watu kujizuia wakati taarifa hiyo ikisambaa hadi pale uchunguzi utakapokamilika.

**DW**

# Russia yaonja moto wa Ukraine

**MOSCOW, Russia**

GAVANA wa Belgorod nchini Russia, amesema watu watatu wameuawa katika shambulio la ndege zisizo na rubani katika kijiji kilicho karibu na mpaka wa Ukraine.

Akichapisha kwenye mtandao wa Telegram Vyacheslav Gladkov, alisema vikosi vya kijeshi vya Ukraine vilirusha kifaa cha kulipuka kupitia ndege isiyo na rubani wakati watu wakiwa mitaani.

Kijiji cha Lavy kiko kilomita 21.51 kaskazini mwa mpaka wa Ukraine na Russia.

Hata hivyo, Ukraine haijatoa taarifa yoyote kuhusu tukio hilo.

Wizara ya Ulinzi ya Russia ilisema ilizuia shambulio la ndege isiyo na rubani ya Ukraine dhidi ya mji wa Moscow usiku kucha wa jana.

Ilisema ndege zisizo na rubani mbili ziliangushwa na ulinzi wa anga; lakini meya wa jiji hilo alisema la tatu liligonga jengo lililokuwa likijengwa.

Safari za ndege katika viwanja vya ndege vitatu vya Sheremetyevo, Domodedovo na Vnukovo vilisitisha huduma kwa muda mfupi.

**BBC**

# BRICS yajadili kuongeza wanachama

**JOHANNESBURG, Afrika Kusini**

MKUTANO wa kilele wa kundi la uchumi wa mataifa yanayoendelea kwa kasi duniani la BRICS, umeingia siku ya pili jana na kutawaliwa na mjadala muhimu wa kutanua ukubwa wa kundi hilo, kwa kuyakaribisha mataifa mengine kuwa wanachama.

Katika siku ya kwanza ya mkutano huo unaofanyika mjini Johannesburg, Afrika Kusini, viongozi wa mataifa hayo ya Brazil, China, India, Afrika Kusini na Russia walitoa hotuba zilizomulika mwelekeo wa kundi hilo la kiuchumi na nafasi yake katika ulimwengu wa sasa.

Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa alielezea matarajio yake kuhusu kundi hilo.

Rais Vladimir Putin wa Russia ambaye alihutubia jukwaa hilo kwa njia ya mtandao, alisema kundi hilo limepiga hatua katika utekelezaji wa dhamira yake ya kuachana na utegemezi wa dola ya Marekani katika biashara na uchumi.

Hotuba za viongozi wengine ikiwemo rais Xi Jinping wa China, ziligusia umuhimu wa kuimarisha nafasi ya kundi la BRICS kwenye Jukwaa la Kimataifa.

Nchi wanachama wa BRICS yanawakilisha robo ya uchumi wa ulimwengu.

**DW**

# SINGIDA FOUNTAIN, PRISONS ZAFUNGUKA WALIPOKWAMA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Singida Fountain Gate, Mathias Lule, amesema suluhu waliyoipata katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Prisons iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Liti, mkoani Singida imetokana na uchovu kwa wachezaji wake.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika, Lule, raia wa Uganda alisema tangu walipocheza mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Ngao ya Jamii dhidi ya Simba, wachezaji wao hawajapata muda wa kupumzika.

Lule alisema wachezaji wao wameshindwa kuonyesha kiwango chao halisi tangu walipocheza pia dhidi ya Azam FC, katika mchezo wa kusaka mshindi wa tatu.

"Nasema tunafatiki, wachezaji hawajapumzika vizuri, kila kitu tumefanya sawa kuelekea mechi hii (dhidi ya Prisons), lakini uchovu ndio umechangia sana kutopata ushindi kwenye mechi ya leo (juzi)," alisema Lule.

Kocha huyo alitaja mapungufu mengine katika mechi hiyo ni kukosekana kwa pasi nzuri za mwisho ambapo amesema watakwenda kulifanyia kazi.

"Tumepoteza baadhi ya nafasi, lakini ninachoona hatujapata au kutengeneza pasi za mwisho, lakini huu ni mwanzo tu wa ligi, tutakwenda kwenye chumba cha marekebisho na uwanja wa mazoezi tukarekebishe mapungufu hayo," Lule alisema. Timu hiyo imetumia siku 11 kucheza mechi nne, mbili za Ngao ya Jamii na moja ya michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika na nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Juzi ilicheza mechi ya kiporo cha Ligi Kuu Bara raundi ya kwanza, ambapo kwa matokeo hayo imeambulia pointi moja ikiwa nyumbani.

Naye Kocha Mkuu wa Prisons, Fred Minziro, alisema nidhamu ya mchezo kwa vijana wake ndiyo iliyoamua mechi hiyo kuwa suluhu.

"Singida wana timu nzuri, wamesajili vizuri sana, tulichofanya ni kuwaruhusu kukaa na mpira kwao, lakini wakifika katikati tunaanza kuwakaba na kuwasumbua, huu mfumo niliutengeneza baada ya kuwaona kwenye mechi za Ngao ya Jamii na Kombe la Shirikisho, vijana wangu wakawa na nidhamu kubwa ya mchezo, wakafuata maagizo yangu mechi ikaisha kwa sare na kama zile nafasi mbili za wazi tungezipata tungemaliza mchezo," alisema Minziro.

# Waamuzi 40 darasani Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAAMUZI wa soka 40 wanatarajia kufanya mtihani wa utimamu wa mwili ifikapo Jumapili kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar wa mwaka 2023/2024, imefahamika.

Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), Waziri Sheha, alisema kati ya waamuzi hao 36 ni wanaume na waliobakia ni wanawake.

Sheka alisema maandalizi yote kuelekea mtihani huo yamekamilika huku akiweka wazi mchakato wa kupima afya utafanyika keshokutwa kwenye Uwanja wa Mao ze Dong.

Alisema mtihani huo utaambatana na masomo ya darasani pamoja na mtihani wa nadharia na vitendo.

**"Msimuu huu tumekusudia kuhakikisha waamuzi wanafanya vizuri katika masomo ya darasani, hasa somo la sheria ili kuhakikisha mapungufu yote ya msimu uliopita yanafanyiwa kazi, tunataka tuanze msimu kwa kupunguza au kuondoa kabisa malalamiko juu ya waamuzi ya kushindwa kutafsiri sheria," Sheha alisema.**

Mwamuzi huyo mstaafu wa kimataifa aliongeza kwa upande wa Pemba, mtihani huo utimamu wa mwili kwa waamuzi utafanyika Septemba 2, mwaka huu.



Kocha Mkuu wa Azam FC, Yousoupha Dabo (kulia), akimpa maelekezo straika wa timu hiyo, Prince Dube kwa ajili ya mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bahir Dar Kenema kutoka Ethiopia itakayochezwa kesho. **PICHA: MATANDAO**

# Mashujaa FC yaanza kutoa vitisho Bara

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Mashujaa FC cha mkoani Kigoma kimesema kimejipanga vyema kwa ajili ya kusaka matokeo chanya katika kila mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara watakayocheza msimu huu, imeelezwa.

Mashujaa FC walianza vizuri msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2023/2024 ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar na kutoka suluhu iliyokutana na Geita Gold FC.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Mashujaa, Abdallah Mohammed 'Bares' alisema anahitaji kuvuna pointi ama katika mechi ya nyumbani au ugenini kwa sababu anahitaji kumaliza katika nafasi za juu.

Bares alisema anatambua ligi ya msimu huu inaushindani lakini mipango waliojiweka ni kushinda kila mechi watakayocheza na hatimaye kufikia malengo.

Alisema wamekuja katika Ligi Kuu Bara kuonyesha ushindani na matarajio yake makubwa ni kuendelea kasi waliyoanza bila kuwadharau wapinzani wao.

"Tumeanza msimu vizuri, matarajio yangu ni kuona kasi tuliyoanza nayo iwe zaidi katika mechi zijazo, tunapoelekea ligi inazidi kuwa ngumu. Mipango yetu ni kufanya vizuri na kuleta ushindani katika ligi hii ili kufikia malengo, mipango hii ni lazima kushinda mechi za nyumbani na ugenini," alisema Bares.

Aliongeza siku 20 ambazo hawatacheza mechi, wachezaji amewapa mapumziko ya siku nne na siku zilizosalia wataendelea kubakia Kigoma kuendelea na mazoezi.

"Tutakuwa na mapumziko ya siku chache, kwa msingi huo wachezaji watabaki kambini (Kigoma), kwa sababu hatukuwa na muda wa kufanya maandalizi tofauti, tutatumia muda huu kuyafanyia kazi mapungufu ya kikosi changu niliyoyaona katika mechi mbili tulizocheza," alisema Bares.

Hata hivyo aliongeza wanaweza kwenda Burundi au kualika timu kutoka taifa hilo kwa ajili ya kupata mechi za kirafiki za kujipima kabla ya kuwakabili Ihefu ya Mbeya.

Mashujaa watakuwa wenyeji dhidi ya Ihefu katika mechi ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Septemba 16, mwaka huu kwenye dimba la Lake Tanganyika, Kigoma.

## ZISIKUPITE

### KUDUS BADO AWINDWA

KLABU West Ham bado ina matumaini ya kumsajili mchezaji wa Ajax, Mohammed Kudus, baada ya ombi lao la awali la kiungo huyo wa kati mwenye umri wa miaka 23 kukataliwa. **(Sky Sports)**

### ANDRE ATAJWA LIVERPOOL

OFA ya Liverpool ya pauni milioni 25.6 kwa ajili ya kiungo wa Brazil, Andre mwenye umri wa miaka 22, imekataliwa na Fluminense ambao wanasitasita kumwachia mchezaji huyo kabla ya kumalizika kwa msimu wao wa ligi Desemba. **(ESPN)**

### CITY YAMWOTA PAQUETA

MANCHESTER City huenda wakafufua nia yao ya pauni milioni 80 ili kumsajili kiungo wa West Ham na Brazil, Lucas Paqueta (25) ifikapo Januari, mara tu uchunguzi wa Chama cha Soka England (FA), kuhusu madai ya ukiukwaji wa sheria ya kamari ya mchezaji huyo kukamilika. **(Sky Sports)**

### AMRABAT AGOMBEWA ULAYA

KLABU ya Fiorentina wamempa kiungo wa Morocco, Sofyan Amrabat mwenye umri wa miaka 27 hadi Ijumaa kuamua kama anataka kusalia katika klabu hiyo huku, Liverpool, Manchester United na Atletico Madrid zikimwania. **(Corriere dello Sport via Football Italia)**

### GRAVENBERCH SOKONI RASMI

MUSTAKABALI wa kiungo wa kati wa Buyern Munich, Mholanzi Ryan Gravenberch anayewaniwa na Liverpool uko mashakani huku klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani (Bundesliga), ikikaribia kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. (The Athletic)

### ARSENAL: GABRIEL HAUZWI

ARSENAL wameifahamisha klabu mojawapo ya Saudi Arabia na Real Madrid kuwa mlinzi wao Mbrazil, Gabriel mwenye umri wa miaka 25 hapatikani. **(Mirror)**

### SILVA AJIFUNGA CITY

BERNARDO Silva mwenye umri wa miaka 29 ametia saini mkataba mpya na Manchester City, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno akijifunga hadi Juni, 2026. **(Fabrizio Romano)**

### LUKAKU ANUKIA ROMA

KOCHA Mkuu wa AS Roma, Lina Souloukou, amesafiri kwa ndege hadi London, na hivyo kuchochea uvumi wa mazungumzo na Chelsea kuhusu mpango wa kumnunua mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30. **(Tuttomercatoweb)**

### CHELSEA, ODOI BASI

KLABU ya Everton imejiondoa katika mpango wa kumnunua winga wa Chelsea na Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 22. (Liverpool Echo)

### BAYINAR ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United inafikiria kumnunua mlinda mlango wa Fenerbahce na Uturuki, Altay Bayindir, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 akiwa na kipengele cha kumuachia cha pauni milioni 4.2. **(Mail)**

### IHEANACHO ASAKWA EPL

MSHAMBULIAJI wa Leicester City, Kelechi Iheanacho, mwenye umri wa miaka 26, ameibuka kama mlengwa mkuu katika kikosi cha Crystal Palace. (Leicestershire Live). **(Mail)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA AFANYIWA UPASUAJI WA MGONGO

**City sasa itamkosa kocha huyo katika mechi zake mbili dhidi...**

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola atakuwa nje ya benchi la Manchester City baada ya kufanyiwa upasuaji wa mgongo, klabu hiyo imethibitisha.

Guardiola mwenye umri wa miaka 52, alifanyiwa upasuaji huko jijini, Barcelona Jumanne iliyopita na atakosa michezo miwili ijayo wakati City itakapocheza dhidi ya Sheffield United na Fulham.

Nafasi yake itachukuliwa na Kocha Msaidizi, Juanma Lillo, hadi atakaporejea baada ya mapumziko ya kimataifa hapo Septemba.

Taarifa iliyotolewa na City mapema wiki hii ilisema: "Pep Guardiola leo (juzi) amefanyiwa upasuaji wa kawaida wa tatizo la mgongo.

"Bosi wa Manchester City amekuwa akisumbuliwa na maumivu makali ya mgongo kwa muda mrefu hivi karibuni, na alisafiri kwa ndege hadi Barcelona kwa ajili ya upasuaji wa dharura uliofanywa na Dk. Mireia Illueca. Upasuaji huo ulifanikiwa.

"Kwa kipindi hiki ambacho hatakuwepo, Kocha Msaidizi, Juanma Lillo, atasimamia ufundishaji wa kikosi cha kwanza kwenye uwanja wa mazoezi na atachukua jukumu hilo hadi Pep atakaporejea. Anatarajiwa kurejea baada ya mapumziko yajayo ya mechi za kimataifa.

"Kila mtu katika Manchester City anamtakia Pep ahueni ya kupona haraka, na tunatazamia kumwona akirejea Manchester hivi karibuni."

City wameanza msimu wao kwa ushindi mfululizo wa Ligi Kuu England dhidi ya Burnley na Newcastle United, pamoja na ushindi wa UEFA Super Cup dhidi ya Sevilla.

Guardiola atakaporejea ataongoza safari ya kuwafuata West Ham United kwa ajili ya mechi itakayochezwa Septemba 16, mwaka huu.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,146,3

MECHI KALI
LUDOGORETS RAZGRAD
VERSUS
AJAX
1 | 4.18
X | 3.89
2 | 1.71

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Nkuba Mandago - 0652 696 XXX
2. Amiri Mrisho - 0654 223 XXX
3. Yusto Nyahenge - 0657 216 XXX
4. Mussa Mwakikono - 0712 508 XXX
5. Julius Julius - 0713 652 XXX
6. Mwanahamisi Mfaume - 0714 046 XXX
7. Maurini Malle - 0714 209 XXX
8. Maulid Mahangaiko - 0718 469 XXX
9. Theonas Ntandu - 0718 738 XXX
10. Joseph Gilla - 0719 503 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MOUNT KUIGHARIMU UNITED, HATIHATI KUIKABILI ARSENAL



**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imethibitisha, Mason Mount atakuwa nje ya uwanja hadi baada ya mapumziko ya kalenda ya kimataifa kutokana na jeraha.

Kiungo huyo alijiunga na United wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto kwa pauni milioni 55 kutoka kwa mahasimu wao wa Ligi Kuu England, Chelsea, akisaini mkataba wa miaka minne, pamoja na chaguo la mwaka zaidi.

Mount ameanza mechi zote mbili za United za Ligi Kuu kwa msimu wa 2023/2024, kwa kuwachapa Wolves mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Old Trafford kabla ya kipigo kutoka kwa Tottenham Hotspur Jumamosi iliyopita huko Kaskazini mwa London.

Katika mchezo wa mwisho, kiungo huyo alitoka nje dakika ya 85 na United sasa wamethibitisha mabadiliko hayo yalitokana na jeraha.

"Mason Mount anatazamiwa kukosa mchezo wa Jumamosi dhidi ya Nottingham Forest kutokana na jeraha alilolipata kwenye mechi ya wikiendi iliyopita dhidi ya Tottenham Hotspur.

"Maumivu hayo madogo yanatarajiwa kumweka Mount nje ya uwanja hadi mapumziko ya kimataifa mwezi ujao.

"Kiungo huyo wa kati wa England ameanza mechi zetu zote mbili za Ligi Kuu England hadi sasa msimu huu baada ya kucheza mechi yake ya kwanza ya ushindani kwenye klabu hiyo katika ushindi wa 1-0 dhidi ya Wolverhampton Wanderers wiki iliyopita Uwanja wa Old Trafford."

Jeraha hilo litaifanya Mount kuikosa Nottingham Forest na safari ya kwenda Uwanja wa Emirates kumenyana na Arsenal.

United imekuwa ikihusishwa na wachezaji kadhaa wa kiungo katika wiki za hivi karibuni, huku 90min wakiripoti United sasa wamekubaliana na Sofyan Amrabat.

# Kadi ya Mac Allister yafutwa

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL watakuwa na Alexis Mac Allister kwa ajili ya mechi zao tatu zijazo za Ligi Kuu England baada ya Chama cha Soka cha England (FA), kuridhia rufaa dhidi ya kadi nyekundu iliyoonyeshwa katika ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Bournemouth walipocheza Jumamosi iliyopita.

Mac Allister alitolewa nje kwa kadi nyekundu na mwamuzi, Thomas Bramall, kwa kumchezea vibaya, Ryan Christie dakika ya 58, jambo ambalo lilimaanisha kiungo huyo wa Argentina alipaswa kukosa mechi dhidi ya Newcastle United, Aston Villa na Wolverhampton Wanderers.



Mac Allister, aliyesajiliwa majira ya joto kutoka Brighton & Hove Albion, alikuwa akicheza mechi yake ya kwanza pale kwenye dimba la Anfield.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, alisema baada ya mechi hiyo klabu itajaribu kubatilishwa kwa kadi hiyo na FA imethibitisha kuwa tume huru ya udhibiti ilikubali kadi hiyo haikuwa sahihi.

Kutolewa kwa kadi nyekundu kulionekana kuwa uamuzi mgumu, huku kocha wa Bournemouth, Andoni Iraola, akisema baada ya mechi hiyo "haikuonekana kama kadi nyekundu."

Klopp alikubaliana na mwenzake, akiiambia Sky Sports: "Ninaelewa kwa asilimia 100 mwamuzi wakati huo hakuona vizuri tukio lile."

## HABARI MICHEZO

# 22,426/-

# AZAM YAJA NA ' LA REVANCHA' KUWAONDOA BAHIR DAR CAF

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuchapwa mabao 2-1 ugenini, Azam FC imesema itaingia katika mechi ya marudiano dhidi ya Bahir Dar Kenema kutoka Ethiopia na kauli mbiu ya 'La Revancha' kwa ajili ya kuhakikisha inapata ushindi na kusonga mbele kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Azam FC itawakaribisha Bahir Dar Kenema kesho na imetamba itapindua meza kibabe katika mechi hiyo ya marudiano.

Ofisa Habari Msaidizi wa Azam, Hasheem Ibwe, alisema matokeo ya mechi ya kwanza yaliwahuzunisha wachezaji wao na sasa wameapa kulipiza kisasi watakapowakaribisha Wahabeshi hao.

"Asante sana Ilunga Idris Mbombo kwa bao lako, limetuweka kwenye sehemu nzuri, tumefungwa mabao 2-1, tumepoteza lakini sio mbaya Chamazi patakuwa patamu, pazito na patawaka moto, nafasi ya kushinda tunayo na kusonga mbele," alisema Ibwe.

Bao la Mbombo linaonekana kuwapa matumaini wawakilishi hao ambapo mshindi wa jumla wa mechi hiyo atakutana na Club Africain ya Tunisia.

Mechi hiyo imepewa jina la 'La Revancha', neno la Kihispaniola linaloomaanisha marudio ya mechi.

Hata hivyo wenyewe Azam FC wamelitafsiri kama ni mechi ya kisasi, huku wakiwataka mashabiki wa timu hiyo pamoja na wengine wajitokeze kwa wingi kwenda kuwaunga mkono.

"La Revancha. Ndio kauli mbiu yetu rasmi kuelekea mchezo wetu wa marudiano dhidi ya Bahir Dar Kenema, ikimaanisha kisasi.

Tukutane kwa wingi Azam Compex Ijumaa hii tutakapoivaa timu hiyo katika mchezo huo wa raundi ya kwanza wa michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, utakaoanza saa 1.00 usiku," alisema kiongozi huyo.



Kocha wa Friends Rangers, Heri Mzozo (kulia), akiwa amejiinamia na wachezaji wake baada ya kuchapwa mabao 5-1 na Kisa katika mechi ya Ligi Kuu ya Ufukweni iliyochezwa hivi karibuni Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# Yanga yakamilisha mawindo ya ASAS

INATOKA UK. 24

Alisema malengo yao ni kuvuka katika hatua inayofuata ingawa anawakubali wapinzani wao wana kikosi bora kilichowapa changamoto kwenye mchezo wa kwanza.

"Tunatambua ASAS FC sio timu ya kuibeza wako vizuri, mechi ya kwanza tuliwafunga ila walionekana wako imara, ninaimani mechi ijayo hawatakuja kama walivyoonekana katika mechi ya kwanza, hii ni kwa sababu wameshajua ubora na madhaifu yetu.

Tumeona pia ubora na mapungufu yao ikiwamo safu ya ulinzi, tutahakikisha yote tuliyoyafanyia kazi yanaonyesha matokeo, hasa katika safu ya ushambuliaji kutumia vyema nafasi tutakazotengeneza na kupata ushindi wa mabao mengi zaidi ya mechi iliyopita," alisema kocha huyo.

Baada ya mechi hiyo ya kimataifa kumalizika, Yanga itawavaa 'Maafande' wa JKT Tanzania katika mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Agosti 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakati watani zao, Simba wenye pointi sita ndio vinara katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

## Robertinho: Sina kikosi cha kwanza

INATOKA UK. 24

Kagabo alisema Kramo aliumia goti wakiwa katika maandalizi ya michuano ya Ngao ya Jamii na hakufanikiwa ama kucheza au kufanya mazoezi magumu mpaka sasa ambapo afya yake imeimarika.

"Sasa hivi anaendelea vizuri baada ya kupewa wiki mbili za mapumziko huku akiwa chini ya uangalizi wangu, tunatarajia Ijumaa (kesho), atashiriki katika mazoezi yenye ushindani," alisema daktari huyo.

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/08/23 | 17:00 | Everton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.26 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/08/23 | 20:00 | Cadiz CF vs UD Almeria | 2.23 | 3.25 | 3.05 |
| 03. 26/08/23 | 20:00 | SC Farense vs GD Chaves | 2.36 | 3.10 | 3.00 |
| 04. 26/08/23 | 20:30 | Granada CF vs RCD Mallorca | 2.55 | 2.90 | 2.95 |
| 05. 26/08/23 | 21:45 | KV Kortrijk vs Standard Liege | 2.95 | 3.45 | 2.21 |
| 06. 26/08/23 | 22:00 | Excelsior Rotterdam vs Fortuna Sittard | 2.22 | 3.50 | 2.90 |
| 07. 27/08/23 | 02:30 | New York Red Bulls vs Inter Miami CF | 2.40 | 3.30 | 2.50 |
| 08. 27/08/23 | 13:15 | PEC Zwolle vs FC Utrecht | 2.90 | 3.60 | 2.21 |
| 09. 27/08/23 | 16:00 | Strasbourg Alsace vs Toulouse FC | 2.09 | 3.50 | 3.20 |
| 10. 27/08/23 | 16:30 | FSV Mainz vs Eintracht Frankfurt | 2.48 | 3.45 | 2.55 |
| 11. 27/08/23 | 17:00 | St. Truidense VV vs Cercle Brugge | 3.05 | 3.30 | 2.23 |
| 12. 27/08/23 | 17:00 | St Mirren FC vs Aberdeen FC | 2.41 | 3.20 | 2.85 |
| 13. 27/08/23 | 17:30 | Boavista Porto vs Casa Pia Lisbon | 2.22 | 3.15 | 3.20 |
| 14. 27/08/23 | 17:45 | SC Heerenveen vs Sparta Rotterdam | 2.26 | 3.50 | 2.85 |
| 15. 27/08/23 | 18:00 | Racing Club de Ferrol vs Sporting Gijon | 2.31 | 3.00 | 3.20 |
| 16. 27/08/23 | 18:00 | Sandefjord Fotball vs FK Haugesund | 2.21 | 3.20 | 2.80 |
| 17. 27/08/23 | 18:30 | Newcastle United vs Liverpool FC | 2.11 | 3.75 | 2.95 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 24/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 1794 | Gaadiidka FC vs APR FC | 7.27 | 3.84 | 1.40 |
| 17:00 | 4686 | Astana vs Partizani Tirana | 1.63 | 3.76 | 5.02 |
| 17:00 | 4725 | Tobol Kostanay vs Viktoria Plzen | 4.11 | 3.51 | 1.81 |
| 17:30 | 3130 | Pakhtakor vs Nasaf Qarshi | 2.55 | 2.95 | 2.55 |
| 17:30 | 4287 | Akademija Pandev vs FK Tikves Kavadarci | 1.99 | 3.16 | 3.57 |
| 18:00 | 4194 | FC Struga Trim Lum vs Breidablik | 2.33 | 3.26 | 2.91 |
| 18:00 | 5511 | AL Tai vs Al Wehda | 2.06 | 3.45 | 3.40 |
| 18:30 | 1786 | TPS Turku vs Hifk | 1.42 | 4.24 | 5.85 |
| 18:50 | 5266 | Al Kuwait SC vs Al Jahra | 1.47 | 4.04 | 5.45 |
| 19:00 | 1495 | Zalgiris vs Ferencvaros TC | 3.76 | 3.41 | 1.92 |
| 19:00 | 2391 | Shabab Alsamu vs Taraji Wadi Al-Nes | 1.99 | 3.43 | 3.18 |
| 19:00 | 4185 | Persepolis FC vs Zob Ahan | 1.33 | 4.18 | 9.38 |
| 19:30 | 5525 | Nordsjalland vs Partizan | 1.57 | 3.86 | 5.41 |
| 20:00 | 2597 | Maccabi Tel Aviv vs NK Celje | 1.40 | 4.40 | 7.20 |
| 20:00 | 2785 | BK Hacken vs Aberdeen | 1.77 | 3.70 | 4.10 |
| 20:00 | 2958 | Levski Sofia vs Eintracht Frankfurt | 6.19 | 4.30 | 1.46 |
| 20:00 | 2985 | Fenerbahce vs Twente | 1.62 | 4.01 | 4.72 |
| 20:00 | 3144 | Farul Constanta vs HJK Helsinki | 1.68 | 3.84 | 4.49 |
| 20:00 | 4061 | Sepsi Osk vs Bodo Glimt | 3.60 | 3.40 | 1.97 |
| 20:00 | 4705 | Dynamo Kiev vs Besiktas | 3.31 | 3.36 | 2.08 |
| 20:00 | 4953 | Slavia Prague vs Zorya Lugansk | 1.20 | 6.19 | 11.98 |
| 20:00 | 5006 | Hobro vs Aalborg | 4.05 | 3.74 | 1.68 |
| 20:00 | 5813 | Rapid Vienna vs Fiorentina | 4.79 | 3.79 | 1.65 |
| 21:00 | 1666 | Al Raed Club vs Al Hilal Riyadh | 12.56 | 6.28 | 1.20 |
| 21:00 | 1789 | Alianza Universidad De Huanuco vs Deportivo Coopsol | 1.43 | 4.24 | 5.65 |
| 21:00 | 2533 | Al Ahli Jeddah vs AL Akhdood | 1.21 | 6.10 | 12.62 |
| 21:00 | 2789 | AL Riyadh vs Al Ittihad Jeddah | 12.62 | 6.10 | 1.21 |
| 21:00 | 3193 | Dinamo Zagreb vs Sparta Prague | 2.15 | 3.25 | 3.25 |
| 21:00 | 3751 | Olimpija Ljubljana vs Karabakh | 2.65 | 3.21 | 2.55 |
| 21:00 | 3780 | Racing Genk vs Adana Demirspor | 1.55 | 4.31 | 4.91 |
| 21:00 | 4556 | Reynir Sandgerdi vs Kormakur/Hvot | 1.78 | 4.02 | 3.46 |
| 21:00 | 4610 | Midtjylland vs Legia Warszawa | 1.93 | 3.49 | 3.64 |
| 21:00 | 4621 | KAA Gent vs Apoel Nicosia | 1.51 | 4.28 | 5.38 |
| 21:00 | 5278 | Lille vs HNK Rijeka | 1.31 | 5.10 | 8.21 |
| 21:00 | 5920 | Ludogorets Razgrad vs Ajax | 4.09 | 3.89 | 1.73 |
| 21:10 | 5120 | AL Nasr vs Kazma SC | 2.73 | 3.28 | 2.28 |
| 21:30 | 2762 | Union Saint Gilloise vs FC Lugano | 1.48 | 4.30 | 5.80 |
| 21:30 | 4200 | FC Maan vs Hussein Irbid | 9.97 | 4.99 | 1.25 |
| 21:30 | 4262 | Osasuna vs Brugge | 2.25 | 3.31 | 3.01 |
| 21:30 | 4507 | Slovan Bratislava vs Aris Limassol | 2.19 | 3.16 | 3.26 |
| 21:45 | 1321 | KF Ballkani vs BATE Borisov | 1.72 | 3.75 | 4.30 |
| 21:45 | 1330 | KI Klaksvik vs Sheriff Tiraspol | 3.31 | 3.26 | 2.12 |
| 21:45 | 4118 | AZ Alkmaar vs Brann | 1.41 | 4.59 | 6.59 |
| 21:45 | 5965 | Hearts vs PAOK | 2.61 | 3.26 | 2.56 |
| 22:00 | 1775 | Olympiakos vs Cukaricki St | 1.24 | 5.22 | 11.71 |
| 22:00 | 2827 | Clube Desportivo Aurora vs CD Real Tomayapo | 1.36 | 4.39 | 7.35 |
| 22:00 | 2988 | LASK Linz vs Zrinjski Mostar | 1.59 | 4.09 | 4.89 |
| 22:00 | 5772 | Always Ready vs Independiente Petrolero | 1.36 | 4.59 | 6.93 |
| 22:15 | 1556 | Augnablik W vs Afturelding Mosfellsbaer W | 9.16 | 7.74 | 1.16 |
| 23:30 | 1587 | Universitario Popayan vs Patriotas FC | 3.66 | 3.05 | 2.00 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

-------------------------
--------

Michezo

Alhamisi Agosti 24, 2023

Nipashe



**Guardiola afanyiwa upasuaji wa mgongo** UKURASA 21




Wachezaji wa Arsenal wakishangilia bao katika mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Crystal Palace iliyochezwa kwenye Uwanja wa Selhurst Park juzi usiku. Arsenal ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAKAMILISHA MAWINDO YA ASAS FC

## Gamondi aitumia KMC kuwapa mbinu mpya mastraika wake...

**Na Saada Akida**

ILI kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amewataka wachezaji wake kusahau ushindi walioupata kwenye mchezo wa kwanza na sasa anahitaji kuona mastraika wanakuwa na njaa ya kufunga mabao.

Yanga ilishinda mabao 2-0 katika mechi yake ya kwanza ya hatua ya awali dhidi ya wenyeji ASAS Djibouti FC na watakutana katika mchezo wa marudiano kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema anautumia mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC kuendelea kuijenga imara safu yake ya ushambuliaji kwa sababu wanahitaji kupata ushindi na kusonga mbele.

Gamondi alisema alitoa maelekezo maalumu kwa washambuliaji wake ambayo anahitaji kuona wanayafanya pia katika mechi dhidi ya ASAS na anaamini wakiyatekeleza wataonyesha kiwango bora cha soka.

Kocha huyo alisema hakuna mechi nyepesi au timu ndogo, soka la sasa limebadilika na amewataka wachezaji wake kuongeza umakini.

"Nahitaji kuona wanafunga mabao, bado hali haijakaa vizuri, kila mechi tunayocheza ni ngumu, ili kujiweka katika nafasi salama ni lazima tufunge, tufunge mabao zaidi ya mawili. Mechi zote za mashindano yote tunayoshiriki ni ngumu na zina ushindani, ni lazima tutumie vizuri kila nafasi tutakayotengeneza," alisema Gamondi.

Aliongeza ili timu ifikie malengo, kila mchezaji anatakiwa kutimiza majukumu yake kutokana na nafasi ambayo anacheza.

"Washambuliaji wetu wameshindwa kufikia malengo ya kufunga idadi kubwa ya mabao mpaka sasa ukilinganisha na namba ya mechi tulizocheza, wamefunga mabao machache ni lazima tubadilishe mfumo ili tuwazidi wapinzani," Gamondi alisema.

Alieleza bado anakiamini kikosi chake na kadri siku zinavyokwenda kinazidi kuimarika kutokana na wachezaji kuanza mazoezi ya Pre Season kwa nyakati tofauti.

INAENDELEA UK. 23

## Robertinho: Sina kikosi cha kwanza

**Na Saada Akida**

LICHA ya kupata ushindi katika mechi zake mbili ilizocheza za Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' amesema bado ataendelea kufanya mabadiliko katika kikosi chake ili kutoa nafasi zaidi kwa wachezaji wake kuzoeana.

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho alisema hasa anataka kuona safu yake ya ulinzi inafahamiana na kuzoeana kwa sababu timu ina mashindano mengi na kila mchezaji anatakiwa kutoa mchango.

Robertinho alisema anahitaji safu yake ya ulinzi iongeze umakini kwa sababu lango linatakiwa kuwa salama wakati wote wa mchezo.

Alisema kuna makosa aliyoyabaini katika safu ya ulinzi kwenye michezo iliyopita baada ya kuumia kwa Mkongomani, Henock Inonga, ambaye tayari alikuwa ameshatengeneza uelewano mzuri na Che Fondoh Malone.

"Baada ya kuumia kwa Inonga, nafasi yake anacheza Kennedy (Juma) pamoja na Che Malone, tunaendelea kufanya mabadiliko ya kikosi taratibu ili wachezaji wazidi kuzoeana. Tuna timu bora lakini tunapaswa kucheza kitimu.

Henock alianza kuzoeana kiuchezaji na Che Malone lakini sasa ameumia, tuna Kennedy na Hussein Kazi, wanafanya vizuri lakini wanapaswa kucheza pamoja mara kwa mara ili wawe bora zaidi," alisema Robertinho.

Aliongeza mabadiliko ya kikosi cha timu hiyo yatafanyika taratibu kwa sababu anaimani ana wachezaji wengi ambao ni wazuri na watakaotoa ushindani kutokana na ubora walionao.

Mbrazil huyo alisema kazi kubwa ambayo anaifanya ni kuimarisha umakini wa kila idara kwa kupata muunganiko ambao utapelekea kila mmoja kuwa tayari kucheza na mwenzake.

Naye Daktari wa Simba, Edwin Kagabo, aliliambia Nipashe nyota wao, Aubin Kramo, anaendelea vizuri baada ya kupewa mapumziko ya wiki mbili na kesho anatarajia kuanza mazoezi ya ushindani pamoja na wachezaji wenzake.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >